epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Novemba 3, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581849
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**MCT** yahimiza kuimarishwa ulinzi waandishi wa habari
UKURASA WA 3



**Rais** Mwinyi asisitiza uwekezaji kukuza ajira
UKURASA WA 8



MAISHA YALIVYO

**Unajua** hatari ndoto unazoota nyakati za usiku?
UKURASA WA 11

RIPOTI MAALUM

# Raia wa China walivyogeuka kuwa machinga Kariakoo



Raia wa China, akifanya biashara ya kuchoma mahindi katika moja ya mitaa ya Kariakoo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**



• **Wafanya** kazi wanapopaswa wazawa, watendaji serikalini watwishwa zigo... *Ukurasa 4*



## Polisi yaanza uchunguzi kupotea kwa bosi Dar24

UKURASA 2

Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu

## Hali ya utegemezi nchini yatisha

UK. 2

MICHEZO **YANGA: HATUJASHUKA KIWANGO** UK.24

**MAONI,** UK.6

**HABARI KITAIFA**

# Jitegemee yatakiwa kuzalisha wahitimu wengi zaidi sayansi

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Tawi la Mafunzo na Operesheni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Meja Jenerali Ibrahim Mhona, katika kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya Shule ya Sekondari Jitegemee JKT, ameitaka kuwa shule bingwa katika uzalishaji wahitimu wa sayansi.

Meja Jenerali Mhona ambaye amemwakilisha Mkuu wa Majeshi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda, alitoa rai hiyo juzi shuleni hapo katika maadhimisho hayo yaliyokwenda sambamba na harambee maalum ya maboresho shule hiyo iliyo chini ya Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMA JKT0.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Meja Jenerali Mhona aliipongeza shule hiyo kwa kutimiza miaka 50 tangu kuanzishwa kwake na kuunga mkono dhamira ya mageuzi inayotaka kufanyiwa shuleni hapo.

Kiongozi huyo alitoa wito kwa walimu kuendeleza viwango vya ubora vya ufaulu shuleni hapo.

"Shule yetu hii katika siku za usoni iwe ni bingwa kutoa watoto wanaokwenda mitaala ya sayansi kwa sababu ukizungumza jeshi ni sayansi, hakuna namna unaweza kupiga bomu mahali usipopaona, kama huna sayansi.

"Halafu huko mbele ili uweze kubagua majeshi rafiki na adui, ili upige kwa adui, inahitajika sayansi. Kama tunazungumza viwanda, maana yake ni sayansi, tukizungumza SUMA JKT ni sayansi. Kule wanafanya ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo, vyote hivyo ni sayansi. Tunawapata wapi watu wa kufanya hizo kazi, ni Jitegemee.

"Shule nzuri ni inayotoa ufaulu. Leo Afande angefurahi sana angekuwapo, huenda angekuwa na maneno mazuri ya kuzungumza kuliko ninayozungumza, bahati mbaya amepatwa na dharura ameshindwa," alisema.

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa SUMA JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alisema uboreshaji wa miundombinu shuleni hapo ni miongoni mwa mikakati ya SUMA JKT.

"Aliyetoa Sh. 100,000 na aliyetoa Sh. milioni 100 wote wametoa sawasawa. Niwashukuru sana, Nimshukuru Afande mgeni rasmi kwa niaba ya Mkuu wa Majeshi ambaye umekuja kumwakilisha, utufukishie salamu zetu. Sisi kama familia ya Jeshi la Kujenga Taifa tumefurahi na tunashukuru," alisema.

"Fedha ambayo mmeahidi kuzichanga na zile mtakazoendelea kuzitoa, mimi ndiye Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, wanaokuja kufanya kazi hii ya ujenzi ni SUMAJKT Construction Co. Ltd, ni kampuni inayofanya majukumu chini ya maelekezo yangu," alisema.

Aliahidi kusimamia jambo hilo ili likamilike kama ambavyo walivyochangia.

Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT, Brigedia Jenerali Petro Ngata, alisema shirika limetekeleza maelekezo ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi kuanza kuboresha miundombinu ya elimu.

"Wazo hili ni sehemu ya maelekezo yaliyotolewa na Afande CDF katika vikao vyake ambavyo amekuwa akivifanya kila mwaka. Sisi kama shirika wenye wajibu wa kusimamia shule hii.

"Tutahakikisha kwamba kile mlichokiona nje katika ubao unaoonesha Jitegemee mpya, tunakuahidi kama wasimamizi, tutahakikisha tunalisimamia hilo ili liweze kuwa bayana na hakika," alisema.

Mkuu wa Shule ya Jitegemee JKT, Kanali Robert Kessy, alisema, "Shule ya Jitegemee JKT imejipatia vijana hodari na wenye nidhamu ambao wanalitumikia taifa katika nyanja mbalimbali."

Katika harambee hiyo, fedha taslimu na ahadi zilizotolewa ni Sh. milioni 501, huku lengo la harambee hiyo, ilikuwa ni Sh. milioni 600.

Sherehe hiyo imehudhuriwa na wakuu wa matawi, wakuu wa vyuo vya kijeshi, wakuu wa kamandi, wakurugenzi SUMAJKT, wakuu wa shule ya Jitegemee JKT wastaafu , taasisi za serikali na binafsi, askari, watumishi wa umma na wahitimu shuleni hapo.

Maadhimisho hayo yalianza kwa kufanyika usafi katika soko la Temeke Stereo, Oktoba 26, mwaka huu, baadaye shughuli ya uchangiaji damu katika Hospitali ya Jeshi Lugalo na kufanyika bonanza lililohusisha michezo mbalimbali.



Mkuu wa Tawi la Mafunzo na Operesheni wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Meja Jenerali Ibrahim Mhona (wa pili kulia), akiangalia picha za namna jengo la Shule ya Sekondari Jitegemee JKT, litakavyokuwa baada ya ujenzi, wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 50 ya shule hiyo, yaliyokwenda sambamba na harambee za ujenzi huo, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hali ya utegemezi nchini yatisha

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imesema watu 87 kati ya 100 ni tegemezi nchini, hivyo kushauri itengwe bajeti ya kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya, ili kupata takwimu ya hali ya umaskini.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Oran Njeza, aliyasema hayo bungeni juzi alipokuwa akisoma maoni ya kamati kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 pamoja na mapendekeo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.

Alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya watu ilikuwa 61,741,120 mwaka 2022 na inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2035 idadi ya watu nchini itakuwa 87,509,630 kutokana na ongezeko la asilimia 3.2 kila mwaka.

"Ongezeko hili la idadi ya watu nchini haliendani na ukuaji wa uchumi. Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba, ongezeko la watu linaendana na ukuaji wa uchumi kwa sababu hivi sasa, kati ya watu 100 watu 87 ni tegemezi,"alisema.

Aidha, alisema kamati inaishauri serikali kutenga bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26, kwa ajili ya kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ili kupata takwimu ya hali ya umaskini nchini kwa kuangalia viashiria vyote 17 kutokana na taarifa iliyoko hivi sasa ya hali ya umaskini ni ya mwaka 2017/18 na imepitwa na wakati.

Alisema Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 ilibainisha kwamba ili Tanzania iondokane na umaskini ni lazima uchumi ukue kwa asilimia nane hadi 10.

"Kamati inashauri kuwa sekta ya kilimo ina uhusiano mkubwa na hali ya umaskini nchini ambapo jumla ya watu milioni 28 sawa na asilimia 45.9 ya watu wote Tanzania wanajishughulisha na sekta ya kilimo.

"Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba, inakamilisha miradi yote ya kilimo kwa wakati ili kupunguza hali ya umaskini nchini. Mfano, mradi wa Kujenga Kesho iliyo Bora (BBT) na ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji," alisema.

**DARAJA LA BUSISI**

Alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha daraja la Kigongo - Busisi linakuwa la kulipia ili kupata fedha zitakazotumika kufanya ukarabati wa daraja hilo.

Alisema kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba, miundombinu ya usambazaji wa umeme inaimarishwa ili kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa wananchi.

"Hivi sasa taifa lina ziada ya umeme wa Megawati 606.04. Hata hivyo, ziada hiyo inaweza kuwa inatokana na wananchi wengi kutounganishwa kwenye gridi ya taifa na kutowafikia wananchi kutokana na ubovu wa miundombinu," alisema.

Njeza alisema kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa sekta ya ujenzi wa barabara inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo utekelezaji kutokuzingatia ujenzi wa barabara za kimkakati, kuanza ujenzi wa barabara nyingi kwa pamoja bila kuzingatia uwezo wa kifedha.

Pia, alisema malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na kusababisha sehemu kubwa ya bajeti kutumika kulipa madeni ya miaka ya nyuma.

Alishauri serikali kutoa kipaumbele katika ujenzi na ukarabati wa barabara za kimkakati na zenye manufaa

# Polisi yaanza uchunguzi kutoweka bosi Dar24

**Na Restuta James**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limesema linamtafuta Mkurugenzi wa Dar24, Maclean Mwaijonga, anayedaiwa kupotea kwa takriban siku nne hadi sasa.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alisema jana kupitia taarifa yake kwa vyombo vya habari kwamba familia yake imeripoti tukio la kupotea kwa Mwaijonga katika Kituo cha Polisi Oysterbay.

Alisema imeripotiwa kwamba Mwaijonga ambaye pia alikuwa mfanyakazi katika Kampuni ya Data Vision International Ltd, iliyoko Mikocheni, Dar es Salaam, hakurudi nyumbani kwake tangu alipoingia kazini Oktoba 31, mwaka huu.

Alisema pia, gari yake namba T 645 DEE, aina ya Toyota Prado, aliyokuwa anaitumia siku hiyo, nayo haionekani.

"Uchunguzi na ufuatiliaji wa taarifa hiyo unafanywa na polisi kwa kushirikiana na ndugu, ili kujua na kubaini mtu huyo yupo wapi.

"Jeshi la Polisi linatoa wito kwa yeyote mwenye taarifa kuhusiana na mtu huyo azitoe katika mamlaka yoyote ya serikali iliyo karibu yake," alisema Kamanda Muliro katika taarifa hiyo.

Awali, kampuni ya Dar24 Media iliripoti kupotea kwa Mwaijonga ambaye hajulikani aliko tangu alipoonekana Oktoba 31, mwaka huu, saa 11:00 jioni alipokuwa akitoka ofisini kwake, DataVision International Ltd, Mikocheni.

Mkurugenzi wa Biashara wa DataVision International, MacMillan George, alisema: "Dar24 Media inaomba atakayemwona au kuwa na taarifa za Mwaijonga au gari lake, atoe taarifa kupitia namba 0713249003."

# Wanaotoa elimu ya ukatili wajikite maeneo pembezoni

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, amewataka wadau wanaotoa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili nchini, kujikita kutoa elimu hiyo katika maeneo ya vijijini ambako wananchi wengi hawafikiwi na taarifa kwa wakati.

Alitoa wito huo Alhmasi wakati akifungua Mpango wa Maandalizi ya Siku 16 za kupinga vitendo vya ukatili zinazoadhimishwa kuanzia Novemba 25 hadi Desemba 10 ya kila mwaka.

Naibu Waziri Mwanaidi, alisema serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kutekeleza afua za kutokomeza ukatili katika jamii na inathamini jitihada zinazofanywa na wadau katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Alisema serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano uliopo kati ya sekta ya umma, binafsi na wadau, kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kijinsia.

Alisema serikali inaendelea kufanya jitihada mbalimbali za kupambana na vitendo vya ukatili ikiwamo kuanzisha madawati ya kupinga ukatili katika vyuo vikuu, vya kati na maeneo ya masoko.

Alisema hadi sasa jumla ya madawati 332 yameanzishwa katika vyuo vya elimu ya juu na elimu ya kati na jumla ya masoko 187 katika mikoa 14 na halmashauri 96 yameanzisha madawati hayo.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wa pili wa MTAKUWWA ambapo miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa awamu ya kwanza, ni pamoja na kuanzishwa kwa kamati 18,186 kati ya 20,750 katika ngazi ya mikoa, halmashauri, kata vijiji na mitaa na jitihada zinaendelea kuhakikisha kamati hizo zinaundwa katika maeneo yote ya nchi.

Alisema serikali inaendelea kushirikiana na wadau katika kuratibu kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini ambapo katika kuunga mkono mapambano hayo, kampeni mbalimbali za ukatili wa kijinsia zimeanzishwa ikiwamo, Zijue Fursa, Imarisha Uchumi, Kataa Ukatili, Kazi Iendelee (ZIFIUKUKI) pamoja na kampeni mbalimbali zinazotekelezwa ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa.

"Niwapongeze wadau mbalimbali wanaotekeleza afua za kutokomeza ukatili hususani Shirika la Blue Cross, Shirika la Mission 21 pamoja na Kanisa la Moravian. Kazi yenu ni njema na itasaidia kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuwa na jamii huru dhidi ya ukatili wa kijinsia," alisema.

Meneja Programu wa Shirika la Blue Cross, Gloria Vincent, alisema shirika hilo limeona umuhimu wa kushirikiana na serikali katika kuifikia jamii kwa kutoa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili kwa kutumia njia mbalimbali hasa kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wa maeneo husika, kimiila na kidini ili kuifikia jamii na kuondokana na vitendo hivyo.

Baadhi ya wadau walioshiriki mkutano wa wadau kuelekea Siku 16 za Kupinga Vitendo vya Ukatili, walisema wapo tayari kufika maeneo ambayo mashirika mengi hayajafika ili kushirikiana na jamii husika kujadiliana na kupata namna bora ya jamii kuondoka na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake watoto na wanaume.



Rais wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Deogratius Nsokolo, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanachama wa UTPC, mjini Singida jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# MCT yahimiza ulinzi waandishi wa habari

**Na Restuta James**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limetoa rai kwa serikali kulinda waandishi wa habari, ili wafanye kazi yao kwa uhuru na hivyo kukuza na kulinda demokrasia.

Aidha, madhila ya waandishi wa habari kukamatwa, vitisho, kutekwa na watu wasiojulikana, chombo cha habari kufungiwa, kipindi kukatishwa kikiwa hewani, kusumbuliwa, kunyimwa taarifa, uhuru wa mahakama kuingiliwa na kunyang'anywa vifaa, yameongezeka nchini, kutoka 19 mwaka juzi hadi 33, mwaka huu.

Katibu Mtendaji wa MCT, Ernest Sungura, aliyaeleza hayo kupitia taarifa yake aliyoitoa jana kwa vyombo vya habari, ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili dhidi ya Waandishi wa Habari (IDEI).

Alisema kati ya mwaka 2012 hadi Oktoba, mwaka huu, waandishi wa habari 316, wamepatwa na madhila ya aina mbalimbali na kwamba, kwa mwaka huu pekee, waandishi 44 wameathiriwa.

Alisema madhila ya kukamatwa kwa waandishi yanaongoza kukiwa na matukio 31, yakifuatiwa na vitisho (8), kutekwa na watu wasiojulikana (1), onyo kwa vyombo vya habari (4), chombo cha habari kufungiwa (4), kipindi kukatishwa kikiwa hewani (1), kusumbuliwa (1), kunyimwa taarifa (1), uhuru wa mahakama kuingiliwa (1) na kunyang'anywa vifaa (1). Kati yao wanaume ni 36 na wanawake ni wanane.

Sungura alisema kwa mujibu wa ripoti ya Taasisi ya Waandishi wa Habari wasio na Mipaka (RSF), Tanzania imepanda katika viwango vya uhuru wa habari kutoka nafasi ya 143 mwaka 2023 hadi nafasi ya 97 mwaka huu.

"Serikali ya Tanzania ina kila sababu ya kuongeza nguvu ya kuwalinda waandishi wa habari dhidi ya madhila, kutokana na kuongezeka kwa madhila dhidi yao kwa mwaka huu, ukilinganisha na miaka miwili iliyopita. Mwaka 2022, madhila 19 yalirekodiwa, mwaka jana, madhila 23 na mwaka huu, hadi leo (jana), madhila 33 yamerekodiwa," alifafanua.

Sungura ambaye pia ni, Mwenyekiti wa Mtandao wa Mabaraza Huru ya Habari Afrika (NIMCA) na Umoja wa Haki ya Kupata Taarifa nchini Tanzania (CoRI), alisema mashirika hayo yanapinga ukatili dhidi ya waandishi wa habari kote duniani.

"CoRI inaunga mkono mazungumzo kati ya serikali na wadau wa habari, katika kujenga mwafaka wa kukabiliana na ukatili dhidi ya waandishi wa habari hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwaka 2025," alisema.

Sungura alisema wiki ijayo, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, watakutana na wadau wa CoRI, chini ya uratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC).

Alisema lengo la kukutana ni kutengeneza mazingira wezeshi na salama kwa waandishi wa habari, ili watekeleze wajibu wao wa kutoa habari, kufichua uovu na kuelimisha umma kwa uhuru, kwa nia ya kujenga demokrasia ya Tanzania.

Katika hatua nyingine, Sungura alisema taarifa za ufuatiliaji za Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), kuhusu ukatili dhidi ya waandishi wa habari, inaonesha kuwa vitendo hivyo ni vikubwa.

Alisema taarifa hiyo inaonesha kwamba kati ya mwaka 2006 hadi 2024, zaidi ya waandishi 1,700 wameuawa duniani na asilimia 90 ya kesi za mauaji hayo hazijatatuliwa mahakamani.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni: Usalama wa waandishi wa habari wakati wa migogoro na dharura.

# Raia wa China walivyogeuka machinga maduka Kariakoo

Na Mwandishi Wetu

UNAPOTEMBEA katika Mitaa ya Agrey, Nyamwezi, Livingstone, Swahili na Congo jijini Dar es Salaam, ni kawaida kuona raia wa kigeni wakifanya kazi ambazo zinapaswa kufanywa na Watanzania na wao kufanya kazi za kitaalamu na uwekezaji.

Raia hao wa China hutumia mbinu mbalimbali zikiwamo kuwa na maduka ambayo huonesha wanauza bidhaa kwa jumla lakini hugeuka kuwa wauzaji wa rejareja na wakati mwingine huchuuza bidhaa kutoka eneo moja hadi jingine.

Hivi karibuni, palizuka mgogoro baina ya raia wa China na Mtanzania wakigombea eneo la kupanga bidhaa. Picha jongefu za tukio hilo zilisambaa kwa kasi kubwa kwenye mitandao ya kijamii hatua iliyomshtua Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye aliagiza mamlaka za serikali kuhakikisha raia wa kigeni wanafanyakazi kwa mujibu wa vibali vyao na kutaka kazi za Watanzania kulindwa.

Pia alimwelekeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo alisema: "Nimeona video Mchina akipigana na mwenyeji tena mwanamke. Mchina mwanamume na mwenyeji mwanamke, ngumu za kweli kweli. Nilipouliza kulikoni, nikaambiwa yule Mchina naye anauza mitumba, biashara ya wenyeji tena wenyeji vijana wetu. Hilo nalo kalitizame.

"Kama biashara haifai kufanywa na watu wa nje wasifanye. Sababu ni nini mpaka wanapewa leseni ya kufanya biashara za aina ile? Na kama hawapewi leseni kwa nini wanafanya biashara za aina ile?"

Mfanyabiashara katika eneo hilo, Yusuf Charles, anasema mwingiliano huo unawagharimu kibiashara kwa kuwa Wachina wanauza kwa bei ya rejareja, tena kwa bei ndogo kuliko wazawa, wana mitaji mikubwa na bidhaa wanazitoa nchini mwao kwa bei ya chini.

Anasema Wachina wanatakiwa waje kama wawekezaji wakubwa, wauze bidhaa zao kwa bei ya jumla, badala ya kuchanganyika sokoni kama machinga. Anasema kujipenyeza kwao katika eneo hilo kumetokana na baadhi ya viongozi wenye mamlaka kutowajibika ipasavyo na kuendekeza rushwa.

"Wapo mpaka waliogeuka kama machinga. Walianza kidogo kidogo sasa wameongezeka. Wengine wanajifanya wana maduka ya jumla lakini ukienda dukani wanauza kwa bei ya rejareja. Ukiingia katika duka la Mchina hata ukitaka kijiko au kikombe kimoja unapata, wakati wanatakiwa kuuza kuanzia dazani moja na kuendelea.

"Ninaona mwingiliano huu kwa sasa kuudhibiti itakuwa ngumu kwa sababu wanajua njia zote za kuikwepa serikali na wanafundishwa na wazawa waliowaajiri katika maduka yao.

"Kingine wanachokifanya kwa kuwa wanajua sheria haiwaruhusu wao kufanya biashara kama wafanyabiashara wadogo, wanatumia kivuli cha wazawa kumiliki maduka ili isiwe rahisi wao kutambulika," anafichua Charles.

Mfanyabiashara mwingine, Rashid Chunga, anasema: "Biashara ambazo ni mahsusi kufanywa na wazawa zinafanywa na Wachina. Hali inazidi kuwa mbaya kwa Watanzania ndiyo maana kila siku malalamiko ya kukosa ajira yanakuwa mengi.

"Wanatuua kibiashara, wanavuruga ushiriki wa wazawa katika kujenga uchumi wa nchi. Kwa sasa tunashuhudia baadhi ya wazawa wanafunga maduka kwa sababu kushindana na Mchina kibiashara si rahisi. Wana mbinu nyingi na wana mitaji mikubwa.

"Ukituuliza leo tunataka nini kuhusu Wachina, nitakwambia tunataka wawe Kimanzichana, Kibaha, Chamazi, Mkuranga. Mfanyabiashara atoke hapa awafuate huko akafunge bidhaa arudi badala ya kuwa nao hapa tena wakiuza kwa rejareja".

Mariam Ngonyani, mfanyabiashara wa mitumba, anasema anaona kuna hasara katika hilo akiwa na ufafanuzi kwamba:

"Wachina hawanunui bidhaa nchini. Kazi yao ni kukusanya fedha zetu na kuzibadilisha kuwa dola halafu wanazipeleka nchini kwao. Ukiangalia kwa picha kubwa unagundua hawasaidii kujenga uchumi wa Tanzania, badala yake wanauvuruga kwa faida yao.

"Waende nje ya mji wasiruhusiwe hata kuwa na maduka ya jumla. Wengi pia wanapitia mwanya huo, baadaye wanaanza kuuza kwa bei ya rejareja. Sasa hivi tunaishi nao wanajua mpaka namna ya kukwepa kodi. Wakati mwingine hata risiti hawatoi.

Irene Nzala, mfanyabiashara wa vifaa vya ujenzi, anafichua njia nyingine wanayotumia kumiliki maduka na kuuza kwa rejareja kuwa ni kuwatafuta wazawa ambao wana mitaji midogo halafu wanakubaliana kufanya biashara pamoja.

"Unakuta ghafla mtu duka lake limejaa. Ukipeleleza vizuri unakuta asilimia 80 ya bidhaa zilizoko ni za Mchina. Wao hawataki kujulikana bali Mchina huyo anaonekana muda wa kufunga hesabu tu," anasema.

Nzala anazishauri mamlaka zinazohusika na viwanda na biashara na mambo ya ndani, kuziba mianya ya leseni na vibali kwa wageni.



Baadhi ya Wachina, wakiwa katika shughuli mbalimbali, mitaa ya Karikaoo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

### VIONGOZI WALONGA

Katibu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Uroki Ombeni, anathibitisha kuwapo kwa changamoto hiyo, akisema kitendo cha Wachina kuingilia biashara za wazawa ni kufanya Watanzania waendelee kubaki maskini na ombaomba.

Anasema kila siku wananchi wanaendelea kutumbukia katika dimbwi la umaskini, serikali inaona lakini hajui kwa nini hakuna hatua zinazochukuliwa na kuonya kuwa hali hiyo itasababisha athari kubwa baadaye.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, anaungana na Ombeni akisema changamoto hiyo ni kubwa ikizingatiwa kwamba asilimia 85 ya bidhaa zinaagizwa China.

Anasema ni ngumu kushindana nao kibiashara kwa kuwa wao (Wachina) wanapata faida mara mbili kwa kuwa wazawa wananunua katika maduka yao na viwanda vyao, lakini wao tena wanapenya huku kwa 'ujanja ujanja' wanafungua maduka na kuuza kwa rejareja.

"Kwa akili ya kawaida hatuwezi kushindana nao kwa sababu, kwanza, bidhaa nyingi zinatoka kwao, wanapata kwa bei ndogo, wanakopeshwa na viwanda vya kwao kwa bei ya chini na riba ndogo ndiyo maana wanauza kwa bei ya chini na kupata faida.

"Kipindi cha nyuma tuliona kulikuwa na mkazo wa kufuatilia vibali lakini kwa sasa si ajabu kuona Mchina yuko dukani anauza na watu wa uhamiaji wanapita, wanaona na hawafanyi kitu chochote. Jambo hili linaleta picha mbaya kwa wananchi hasa wafanyabiashara dhidi ya serikali yao," anasema.

Pia anasema kuna ujanja mwingine wanaotumia wachina wa kuingia ubia na wazawa na kuwaweka mbele ya biashara zao. Anasema baadhi ya maduka yanauza bidhaa kwa bei ya rejareja, lakini yanamilikiwa na Wachina.

Mwenyekiti huyo, anashauri suala hilo lidhibitiwe mapema,kwa kuwa baadaye wakiwa wengi itakuwa ngumu kuwaondoa.

"Yataanza mambo ya kidiplomasia, itaonekana tunavunja haki za biandamu, lakini sisi lazima tuthamini vya kwetu, kwa sababu hata wao wako makini kulinda vya kwao na wanauzalendo mkubwa.

### HALI KWINGINEKO

Uchunguzi wa gazeti uliofanywa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki , unaonesha kuwa huko kwingine kuna udhibiti mkubwa dhidi ya wageni kufanya biashara ambazo zinaweza kufanywa na wazawa.

Mamlaka za Tanzania zinapawa kulinda wananchi dhidi ya wageni wanaoingia na kuchukua kazi ambazo zinaweza kufanywa na wazawa. Jambo hilo likiachwa linaweza kutengeneza bomu ambalo haitakuwa rahisi kulidhibiti.

"Sisi tunapenda wachina waje na ujuzi tuige teknolojia yao. Waje kama wawekezaji lakini si kama ilivyo kwa sasa Kariakoo," anashauri.

Mbwana anashauri Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya ziara katika eneo hilo na wako tayari kuwapa ushirikiano na iundwe timu ya pamoja kwa ajili ya kufuatilia suala hilo.

Kutokana na kuwapo wafanyabiashara hao raia wa China, Mbwana anasema ameshuluhisha migogoro mitatu ofisini kwake baina yao na wazawa hali ambayo inatoa ishara kwamba mbele si shwari.

Ofisa Biashara wa Jiji la Dar es Salaam, Nicas Msemwa, anasema suala hilo haliko kwa Wachina pekee nali watu kutoka mataifa mbalimbali ambao wako katika mitaa anuai wakifanya biashara kama hizo.

"Leseni tunazowapatia zinaelekeza wawe wafanyabiashara wa jumla si rejareja. Tuliwahi kupata hayo malalamiko tukawaandikia barua jumuiya ya wafanyabiashara tukawauliza kama wanawafahamu hao watu na watupe majina yao na waliseme hawawafahamu.

"Tumefanya kazi na wahusika na hajaonekana mtu kama huyo. Rai yangu kila mfanyabiashara afanye biashara kulingana na leseni aliyo nayo," anasisitiza Msemwa.

Mwandishi wa Habari hii alipita katika maduka hayo askijifanya mhitaji wa bidhaa katika baadhi ya maduka ya Wachina na kubaini kwamba wengi wanauza rejareja.

### MADHARA KIUCHUMI

Mtaalamu wa masuala ya fedha na Mkuu wa Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Prof. Marcelina Chijoriga, anasema mwingiliano huo una athari za moja kwa moja katika uchumi wa nchi.

"Kisera si sawa wageni kufanya kazi zinazoweza kufanywa na Watanzania. Jambo hili lina athari za moja kwa moja kiuchumi kwamba wafanyabiashara wa Kitanzania watakosa kipato," anasema.

## HABARI KITAIFA




Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wakizima moto uliokuwa ukiteketeza nyumba iliyokuwa na wafanyabiashara ya magororo katika Mtaa wa Kipati Kariakoo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Deni la serikali lafikia tril. 97/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imesema hadi Juni 2024, deni la serikali lilikuwa Sh. trilioni 96.88 ikilinganishwa na Sh. trilioni 81.98 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 18.18.

Aidha, imeishauri serikali mambo manne ya kuhakikisha deni la serikali linaendelea kuwa himilivu.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Oran Njeza, aliyasema hayo bungeni juzi alipokuwa akisoma maoni ya kamati kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 pamoja na mapendekeo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya serikali kwa Mwaka 2025/26.

Alisema ongezeko hilo la asilimia 18.18 ni sawa na Sh. trilioni 14.90 na kati ya deni hilo la ndani lilikuwa Sh. trilioni 31.95 na nje lilikuwa Sh. trilioni 64.93. "Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mpaka sasa deni la serikali ni himilivu kwa kipindi kifupi, cha kati na kirefu. Ongezeko la deni limesababishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi pamoja na kupokea mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo," alisema.

Hata hivyo, alisema kamati hiyo inashauri serikali kuongeza wigo na ukusanyaji wa mapato ya ndani ili yawe na uwezo wa kugharamia deni, mikopo yote inayopatikana ni vema serikali ikaielekeza katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

Alisema lengo ni kuhakikisha hawafiki katika ukomo wa ulipaji wa deni la nje kwa uuzaji wa bidhaa nje ambao hivi sasa tupo asilimia 11.1 na ukomo ni asilimia 15.

"Kutoa kipaumbele kwa mikopo yenye masharti nafuu na yenye masharti ya kati ili kupunguza mzigo wa riba pamoja na muda mfupi wa neema ambao unaambatana na mikopo ya kibiashara na kutafuta vyanzo vingine bunifu vya mapato kama vile hatifungani za kijani, diaspora, manispaa na miundombinu," alisema. Akizungumzia hali ya umaskini na maendeleo ya watu, Njeza alisema kamati inaishauri serikali kutenga bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26, kwa ajili ya kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ili kupata takwimu ya hali ya umaskini nchini kwa kuwa taarifa ya mwaka 2017/18 imepitwa na wakati.

"Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kwamba, ongezeko la watu linaendana na ukuaji wa uchumi kwa sababu, hivi sasa kati ya watu 100 watu 87 ni tegemezi," alisema.

**SGR NA MGR**

Alisema kamati inashauri kutenganisha usimamizi wa reli ya Kisasa ya SGR na reli ya MGR na kulifanya Shirika la Reli nchini (TRC) kuwa Shirika Hodhi linalosimamia Mashirika mawili.

"Serikali itumie mpango wa kufadhili ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR kwa kutumia ECGA (Export Credit Guarantee Agency) ili kukamilisha vipande vyote vilivyobaki kwa haraka hususan vipande vya Uvinza - Malagarasi-Msongati na Kaliua- Mpanda-Karema," alisema.

Alisema kamati inaishauri serikali, kuongeza safari za ndege katika maeneo ambayo wana uhusiano mkubwa wa kibiashara, sambamba na kuboresha viwanja vya ndege vya ndani kwa kuviwekea taa, ili kuongeza idadi ya miruko ya ndege za ATCL ndani ya nchi.

## Othman kufikisha changamoto soko la Tandika kwa Samia

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema mazingira ya soko la wafanyabiashara wa matunda na nafaka la Tandika hayaakisi mahitaji sahihi ya soko kutokana na uchakavu wa miundombinu na uchafu.

Amewaahidi wafanyabiashara sokoni hapo kuwasilisha malalamiko yao kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ili kuchukuliwa hatua sahihi za kurekebisha mazingira hayo ya kufanyia biashara kuwa rafiki.

Othman ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT- Wazalendo alitoa ahadi hiyo baada ya kutembelea soko hilo lililoko wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam, kuona shughuli za kibiashara na hali ilivyo sokoni hapo.

Alisema pamoja na mahitaji makubwa yaliyoko kwa wafanyabiashara na wananchi katika kulitumia soko hilo, lakini mazingira yake hayafanani na soko hilo, jambo ambalo linaweza kuwasababishia matatizo na madhara makubwa ya kiafya, kutokana mazingira kuwa machafu.

Soko hilo, alisema halina miundombinu muhimu ya kibiashara ikiwamo njia za kutirika maji machafu, huku lenyewe likiwa katika hali ya uchakavu, jambo linaweza kusababisha madhara iwapo hatua za kurekebisha hazitachukuliwa. Othman alisema hali hiyo iwapo haitachukiwa hatua stahiki, kuna uwezekano serikali ikapata hasara kwa kuendelea kutibu maradhi yatokanayo na uchafu wa bidhaa zinazotoka katika soko hilo.

Wafanyabiashara wa soko la Tandika walimweleza kiongozi huyo changamoto kubwa zilizoko sokoni hapo ni kipindi cha mvua paa kuvuja, kukosa miundombinu ya maji machafu, jambo ambalo linawaletea usumbufu wa kuendesha shughuli zao.

Katika ziara yake maeneo mbalimbali mkoani humo, Othman aliwataka wananchi kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kwa sababu ndio jukwaa sahihi la kuleta mageuzi ya kisasa ya uongozi nchini.

# Nyumba za Wajerumani Zanzibar zamwibua Karume

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba Zanzibar (ZHC) limedaiwa kukosea kuwataka wakazi wa nyumba za Mjeruamani zilizoko Kikwajuni, kuhama kabla ya nyumba hizo kuvunjwa kupisha uwekezaji, likidaiwa majengo hayo si mali ya ZHC.

Mvutano huo umewaibua watu kadhaa akiwamo mtoto wa pili wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Balozi Ali Abeid Karume, ambaye ndiye aliyebariki ujenzi wa makazi hayo.

Aidha, umemwibua pia aliyekuwa Mbunge wa Kikwajuni, Parmukh Hoogan Sigh.

Balozi Karume alisema kitendo kitakachofanya wananchi wanaoishi katika nyumba hizo kuhamishwa kinaweza kuzua mtafaruku.

"Majengo ya mjerumani si miliki ya Shirika la Nyumba Zanzibar bali yako chini ya dhamana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Yamejengwa na Ujerumani ili wananchi wanyonge waishi. Madai yoyote ya kuwaondoa wakazi wake yanaweza kutaleta hekaheka kubwa," alisema.

Singh alisema kuvunjwa nyumba hizo kutafuta historia kati ya Ujerumani na Zanzibar kwa sababu ndiyo waliojenga baada ya Mapinduzi.

Ujerumani Mashariki ndiyo taifa la kwanza kuyatambua mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964, ikafuatia China kabla ya mataifa mengine duniani kufanya hivyo.

"Majengo yale yana siasa kwa upande mmoja, pia historia na utalii. Kuyavunja na kubadilisha matumizi ni kuvuruga uhusiano na ushirikiano. Ni vema ikashauri Ujerumani ili ivunje na kujenga mengine kuliko kufuta alama yao kihistoria," alisema Singh. Aliongeza kuwa itakuwa busara Ujerumani ikashirikishwa mapema, kwani hata kiongozi wake alitembelea Zanzibar.

Mwenyekiti wa kamati ya kufuatilia mgogoro huo, Jaha Ame Rajab, alisema tayari wananchi wameanza vikao vya kujadili suala hilo na viongozi wa SMZ.

Jaha alisema Mkuu wa Wilaya ya Mjini ameshakutana na kamati yake, hivyo kuna vikao vinavyoendelea ambavyo bado haijajulikana hatima yake.

"Kuna familia nyingi zinaishi katika majengo ya Mjerumani. Kuziondoa familia hizo iki kupisha uwekezaji si jambo la kufumba na kufumbua macho wala kuchukuliwa kwa pupa," alisema Jaha.

Alikumbusha kuwa watu wanaishi tangu awamu ya kwanza, hivyo uamuzi wowote wa kuwafukuza, unaweza kuleta manung'uniko yasiokwisha na kushangaza.

Aidha, Chama cha ACT Wazalendo kilisema uamuzi huo unakwenda kinyume na malengo ya Abedi Amani Karume ya kuwapatia wananchi makazi bora. Waziri Kivuli wa Ardhi, Maji, Nishati wa ACT Wazalendo, Rashid Ali Abdalllah, alisema kinachoendelea katika majengo hayo si jambo jema.

"Yawapo mazungumzo kati ya wakazi na SMZ. Ikiwa ni fidia walipwe na kama kutakiwa kuhama hadi ujenzi utakapokamilika wapewe fedha za kujikimu kimaisha si kuwaondoa kinyume na utu wa mtu" alisema Abdallah.

Ghorofa za Kikwajuni zilijengwa baada ya mapinduzi kama msaada wa kuwapatia makazi bora wananchi kazi iliyofanywa na Serikali ya Ujerumani Mashariki.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sheria udhibiti ajira kwa wageni iongezewe meno

**SERIKALI** imekuwa ikisisitiza kuongezwa kwa kasi ya uwekezaji kwa lengo la kukuza uchumi na kutoa ajira kwa vijana wa Tanzania. Msisitizo huo umeleta matokeo chanya kutokana na kampuni mbalimbali za kigeni kuingia nchini na kuwekeza kwa kujenga viwanda na kufungua biashara za bidhaa kutoka mataifa mbalimbali.

Mbali na kuwapo kwa kampuni na wafanyabiashara kutoka nje ya nchi, pia kumekuwa na wazawa wanaoibuka kwa kuanzisha viwanda na biashara kubwa sambamba na wale wanaoagiza bidhaa kutoka mataifa ya nje na kuuza katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika kuhakikisha biashara na uwekezaji vimekuwa na manufaa, taasisi za utoaji vibali kwa ajili ya uwekezaji na sheria zilizokuwa vikwazo pamoja na tozo utitiri vilivyokuwa vikilalamikiwa na wafanyabiashara vimeondolewa. Huduma zote kama vile usajili, vibali vya uwekezaji, masuala ya kodi sasa zinatolewa katika sehemu moja tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

Kwa ujumla, kumekuwa na kufurika kwa bidhaa za ndani na za nje katika miji mbalimbali ikiwamo mikubwa kama vile Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma na Mbeya.

Bidhaa za kila aina zinapatikana takribani miji yote mikubwa na midogo Tanzania, hivyo kuibuliwa kwa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja miongoni mwa vijana wa Tanzania. Kwa mantiki hiyo, umaskini wa kipato miongoni mwa vijana wa Kitanzania na hivyo mzunguko wa fedha mitaani kwa kiasi fulani umeanza kuonekana.

Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazawa kwamba wanaoitwa wawekezaji au wafanyabisahra wakubwa kutoka nje ya nchi kama vile China, wanafanya kazi au biashara ambazo wanapaswa kufanya wafanyabiashara wadogo tena wazawa.

Hivyo ndivyo ambavyo imekuwa ikisisitizwa na serikali kwamba wageni wanaokuja nchini wasiruhusiwe kufanya kazi ndogo zinazoweza kufanywa na wazawa. Hata kwa kada za wataalaamu kuna sheria ambayo inakataza kada mbalimbali ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania kutofanywa na raia wa kigeni.

Pamoja na msisitizo huo, hali imekuwa tofauti kwa sababu wako hata maofisa wa ngazi za chini kutoka nje wanafanya kazi ambazo Watanzania wengi wana uwezo na sifa za kuzifanya. Inashangaza kuona hata wahasibu na maofisa wa taaluma mbalimbali wanaingia na kufanya kazi ambazo wako vijana wengi wa Kitanzania ambao wana uwezo na ujuzi wa kuzifanya.

Katika sekta ya biashara, kwa mfano, imekuwa ikisisitizwa kuwa wafanyabiashara wa nje wanaoingia nchini, wanatakiwa kufanya biashara za jumla kwa kuwauzia wafanyabiashara wadogo. Kinyume chake, wako wafanyabiashara wa kigeni wanaouza bidhaa za rejareja kama wale wadogo jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa na wafanyabiashara wengi.

Katika eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, kwa mfano, kuna raia wa mataifa mbalimbali, wakiwamo kutoka China ambao wana maduka ya bidhaa za jumla na rejareja huku maofisa wa serikali waliopewa jukumu la kusimamia sheria za biashara na uwekezaji wakiwa kimya.

Jambo hilo limesababisha migogoro baina ya wafanyabiashara hao wa kigeni na wazawa kiasi cha baadhi ya matukio kurushwa katika mitandao ya kijamii. Mbali na migogoro hiyo, kuwapo kwa watu kama hao kutoka nje, kunatishia kudumaa kiuchumi kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati wa Tanzania.

Ni vyema jambo hilo likaangaliwa kwa jicho la kipekee kabla ya kusababisha madhara kwa wazawa. Kama kuna sheria zinazosimamia masuala ya biashara na uwekezaji zitekelezwe na kama kuna ulegevu, zipewe meno zaidi ili zing'ate.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kujenga holela ni kukwamisha zimamoto wakati wa majanga

Na Sabato Kasika

**RIPOTI** ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa miaka ya 2020/2021 na 2022/2023 inabainisha vikwazo mbalimbali vinavyolikabili Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ikiwamo mipango miji.

Sababu nyingine inayotajwa ni miundombinu ikiwamo ya barabara kutokuwa rafiki na hivyo kukwamisha jeshi hilo kuwahi kufika kwenye eneo la tukio linapotokea janga la moto.

Yako mengi ambayo CAG anaeleza katika ripoti yake kuhusu vikwazo wakati wa majanga hasa ya moto, lakini nataka nijikite zaidi kwenye suala la ujenzi holela unaoendelea katika maeneo mbalimbali ya mijini.

Jeshi hilo limekuwa likilalamikiwa na jamii kwa mambo mawili, mojawapo ikiwa ni kuchelewa kufika kwenye matukio na pia kutokuwa na maji ya kutosha kwa ajili ya kuzima moto.

Lawama hizo wanasukumiwa Zimamoto, kutokana na kwamba, wakati mwingine ni kweli huwa hawana maji ya kutosha na hivyo, kusababisha jenga au majengo kuteketea bila msaada kutoka kwao.

Ni katika mazingira hayo, askari wa jeshi hilo huwa wanatishiwa kupigwa na wananchi wenye hasira kwa kutokuwa na maji ya kutosha au kuchelewa kufika eneo la tukio.

Pamoja na hayo, ninadhani kuna haja ya kutafakari kwa kina kuhusu ujenzi holela jinsi unavyochangia ukosefu wa barabara za kuwezesha magari ya Zimamoto kuwahi kwenye tukio.

Maeneo mengi ya mijini ikiwamo Dar es Salaam, watu wamejnga nyumba kiholela bila kuacha sehemu ya barabara, badala yake wanaacha vinjia vidogo ambavyo magari hayawezi kupita.

Kwa mtindo huo, linapotokea janga la kuungua nyumba, inakuwa vigumu Zimamoto kufika katika eneo la tukio. Lakini pia hata kukiwa na barabara, wanaweza kuchelewa kutokana na foleni za magari.

Mfano Dar es Salaam, barabara zake huwa zina foleni nyingi za magari, vilevile baadhi ya wakazi wake wamejenga nyumba kiholela, kitendo ambacho wakati wa majanga ni vigumu kupata msaada haraka.

> **Hivyo, ni vyema sasa jamii nayo ijue umuhimu wa kutojenga nyumba kiholela, badala yake nyumba ziwe katika mpangilio ambao unawezesha kuwapo kwa barabara, sio uchochoro ambao magari hayawezi kupita.**

Hivyo, ni vyema sasa jamii nayo ijue umuhimu wa kutojenga nyumba kiholela, badala yake nyumba ziwe katika mpangilio ambao unawezesha kuwapo kwa barabara, sio uchochoro ambao magari hayawezi kupita.

Kwa ujumla Zimamoto wana kasoro zao na jamii nayo ina kasoro zake. Hivyo, kila upande utatue kasoro hizo ili kuondoa lawama zisizo za lazima wakati majanga yanapotokea.

Zimamoto wawe na maji wanapofika kwenye tukio, lakini jamii nayo ijitahidi kujenga nyumba na kuacha barabara maeneo yaweze kufikika kirahisi kuliko ilivyo sasa, gari linakosa sehemu ya kupita na kushindwa kutoa huduma.

Ukosefu wa barabara husababisha magari ya Zimamoto kusimama hata umbali wa mita 100 au kukwama kutoa huduma, kitendo ambacho kama ni nyumba inaungua, inakuwa vigumu kuzima moto.

Ikumbukwe gari la Zimamoto linapokuwa mbali, hata presha ya maji inakuwa ndogo, kazi ya kuzima moto inaweza kuwa ngumu, hivyo, ni vyema kutafakari na kuchukua hatua za kujenga makazi yanayofikika wakati wote, ili majanga yanapotokea yatatuliwe kwa wakati bila kuleta madhara.

Hayo yakifanyika, ninaamini hakutakuwa na lawama tena kwa jeshi hilo ambazo huwa zinatolewa na wananchi zikiwamo za kutofika kwa wakati kwenye tukio, halina maji ya kutosha au maji yaliyopo pesha kubwa.

Suala la kutofika kwa wakati linaweza juu ya uwezo wa jeshi hilo, hasa kutokana na kikwazo cha foleni za magari maeneo ya mijini ikiwamo Dar es Salaam. Lakini kutokuwa na maji ya kutosha kwenye tukio au ujenzi holela, viko ndani ya uwezo wa zimamoto na wananchi wenyewe.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Bunge litimize wajibu wake kikamilifu



Pascal Mayalla

WIKI mbili zilizopita kwenye safu hii, niliandika mada ya kumpongeza Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kwa kazi nzuri aliyoifanya kwenye Mabunge ya Dunia (IPU) kwa kuwakoromea maspika wenzake wa nchi za mabeberu kuziburuza nchi za Afrika.

Nikamuomba Spika Dk. Tulia, atumie nguvu ile ile katika kuliendesha Bunge letu litimize majukumu yake kikamilifu, ikiwamo kutunga sheria na kuisimamia serikali kikamilifu.

Bunge ndicho chombo kikuu cha uwakilishi wa wananchi. Bunge likisema ni wananchi wamesema na kazi kuu ya Bunge ni kutunga sheria na kuisimamamia serikali.

Makala ya leo ni maswali kuhusu mhimili wa Bunge na mhimili wa Mahakama. Je Bunge letu linatunga kweli sheria au linapitisha miswada ya sheria inayotungwa na serikali? Kwa nini mhimili wa Mahakama unaliogopa hivi Bunge?

Msingi wa maswali haya ni mwendelezo wa kuwaelimisha Watanzania kuhusu katiba, sheria na haki kwa dhima ya mtunga katiba alidhamiria nini.

**MIHIMILI MITATU**

Tumerithi utaratibu wa uendeshaji wa nchi kupitia mihimili mitatu ya Utawala (serikali) Bunge na Mahakama kutoka kwa Waingereza. Utaratubu huu una kanuni zake. Sisi tumeiga uendeshaji tu lakini hatufuati kanuni zake.

Mhimili hii inaongozwa na wakuu wa mihimili, Serikali ikiongozwa na Rais, Bunge likiongozwa na Spika na Mahakama na Jaji Mkuu.

Kila mhimili una kazi zake, majukumu yake, mamlaka yake, madaraka yake na mipaka yake ambayo haipaswi kuingiliana.

Kwa mujibu wa muundo wa mihimili hii, kinadharia inapaswa kuwa sawa. Hakuna mhimili mkubwa wala mhimili mdogo, yote ina haki sawa.

Mihimili hii inapaswa kila mmoja kuwa huru kutoingiliwa na mhimili mwingine na kuheshimiama baina ya mihimili katika kanuni inayoitwa kwa kizungu 'The Doctrine of Separation of Powers, Checks and Balance'.

Hii ni kanuni ya kila mhimili kuwa huru lakini pia kila mhimili ni kiranja wa mwenzake. Huu ukiranja wa mihimili Tanzania ni kama haupo.

Tukianzia na jukumu la Bunge kutunga sheria, si mara moja wala mbili mnasikia Mahakama imebatilisha sheria fulani kwa kwenda kinyume cha Katiba.

Hiyo maana yake ni Bunge limetunga sheria batili. Kwa vile kuna kanuni ya mihimili kuheshimiana, Mahakama inabatilisha tu sheria batili zinazotungwa na Bunge bila kuliuliza Bunge linawazaje kutunga sheria batili, huku limeshehenezwa na wanasheria nguli, wabobezi na wabebovu?. Ukiranja ungekuwepo, hili lisingetokea.

Jibu ni moja tu, Bunge letu halitungi sheria. Miswada ya sheria inatungwa na serikali na kupelekwa Bungeni ijadiliwe na kupitishwa kuwa sheria. Kitendo cha Bunge kujadili miswada hiyo na kupitishwa, ndiko kunakohesabiwa ni Bunge kutunga sheria.

Kwa maoni yangu, Bunge linatumika tu kama 'rubber stsmp' (muhuri) kuipitisha miswada ya sheria inayotungwa na serikali, hivyo anayetunga miswada batili ni serikali yetu tukufu.

Kutokana na kule kule kuheshimiana kwa mihimili, serikali inatunga muswada wa sheria batili, Bunge linapitisha na kuitunga sheria batili na rais wetu analetewa sheria batili na kuzitia saini kuanza kutumika.

Katika hili la Bunge kutunga sheria batili, sheria ya uchaguzi iliyopita ilikuwa pia sheria batili kwa kwenda kinyume cha katiba.

Mahakama Kuu ikaibatilisha, serikali ikakata rufani kupinga kubatilishwa huko, ikashindwa na serikali ikapeleke bungeni mabadiliko batili ya katiba kwa hati ya dharura na kukichomekea kiubatili kipengele batili ndani ya Katiba yetu ili kuihalalisha ile sheria batili kuwa ni sheria halali kwa sababu sasa iko rasmi ndani ya Katiba yetu!

Mahakama Kuu ikagomea serikali kwa kushikilia msimamo kuwa sheria ya uchaguzi ni batili na mabadiliko ya katiba, yaliyofanywa na Bunge, kuichomekea batili hiyo ndani ya Katiba pia ni batili!. Kitendo cha kuichomekea sheria batili ndani ya Katiba yetu, na sawa na kuinajisi Katiba.

Serikali ikakata rufaa Mahakama ya Rufani na kesi kusikilizwa na majaji watu, kisheria inaitwa 'half bench'. Mahakama ya Rufani, kwanza ikaunga mkono uamuzi wa mahakama kuu kuwa sheria ya uchaguzi ni batili na mabadiliko ya katiba yaliyofanywa na Bunge, kuichomekea batili hiyo ndani ya katiba yetu pia ni batili.

Ndipo serikali ikaomba kufanya mapitio Mahakama ya Rufani, ikakaa na majaji saba, kitaalamu 'full bench' chini ya Jaji Mkuu mwenyewe wa wakati huo.

Tena Mahakama ya Rufani, haikukaa peke yake, ikawaita mabingwa watatu wa sheria kuwa marafiki ya mahakama (amicus curiae).

Mahakama ya Rufani ikatoa uamuzi kwa kusema "The court is not the custodians of the will of the people! But the parliament" kumaanisha mhimili wa Mahakama si mlinzi wa matakwa ya watu, huo ni wajibu wa Bunge".

Huku ndiko mimi ninakokuita ni Mhimili wa Mahakama kuligwaya Bunge! Japo ni kweli Bunge ndicho chombo kikuu cha uwakilishi wa wananchi, Mahakama ndiyo mlinzi wa Katiba ya nchi, kumaanisha mhimili wa Mahakama ndio mlinzi wa Katiba, mwenye jukumu la kufsiri katiba na sheria.

Kitendo cha Bunge litunge sheria batili kinyume cha Katiba, kisha lifanye mabadiliko batili ya Katiba, liuchomekee ubatili ndani Katiba yetu ili kuihalalisha ile sheria batili kuwa ni sheria halali kwa sababu sasa iko ndani ya Katiba yetu, hakikupaswa kuachwa hivi hivi.

Badala ya Mahakama ya Rufani kuangalia ubatili wa Katiba na ubatili wa sheria uliofanywa na Bunge, kama mamlaka pekee ya kutafsiri sheria, ilipaswa kuliamuru Bunge kuwa halina uwezo wa kutunga sheria batili wala uwezo wa kufanya mabadiliko batili ya Katiba.

Kitendo cha Mahakama ya Rufani kulirudisha hili suala bungeni, Bunge ndilo liuondoe huo ubatili, kimesababisha ubatili huo kuwa bado ungalipo ndani ya Katiba yetu mpaka leo.

Na hii sheria yetu mpya ya uchaguzi iliyotungwa mwaka huu, umekitumia kipengele hicho batili, hivyo tumetungiwa sheria mpya ya uchaguzi yenye ubatili ule ule ambao ulikwisha batilishwa na Mahakama.

Bunge litimize wajibu wake kikamilifu ikiwemo kutunga sheria, kuisimamia serikali na kuiheshimu Mahakama na Mahakama itemize wajibu wake kikamilifu, iliheshimu Bunge. Isiliogope Bunge linapovunja Katiba. Mahakama iliamuru na si kulibembeleza Bunge eti liondoe ubatili wa Katiba na sheria.

**Paskali**
**+255 754 270403**

KONA YA AFYA

# Namna ya kujikinga na kiharusi



Na Dk. Mabula Budodi

SIKUJUA kama nitakuwa mhanga (mwathirika) wa kiharusi." Alisikika mgonjwa mwenye miaka 45 mwenye familia ya watoto wawili na mume aliyepata ahueni na kuweza kuongea kidogo huku akiwa hawezi kutembea kabisa katika kitengo cha dharura usiku wa manane.

"Nilikuwa nadhania kiharusi kinawapata watu wazee tu wenye umri kuanzia miaka 60 na zaidi. Nilivyokuwa napima mara nyingi na kukutwa na tatizo la shinikizo la damu, madaktari walinishauri kuanza kutumia dawa za kushusha shinikizo la damu na kubadilisha mfumo wangu wa maisha lakini sikutaka hata kusikia.

Ni kama wiki moja kabla ya kupata tatizo hili, alisema alianza kujisikia ovyo ovyo kwa kuanza kupata maumivu makali sana ya kichwa yasiyopoa hata kwa dawa ya kichwa, pia alianza kuona kizungu zungu kikali na hata kutokuona vizuri, yani uhafifu wa kuona uliongezeka siku baada ya siku bila ya kujua sababu ni nini.

Kutoana na hali hiyo, anasema aliishia tu kwenda dukani kununua dawa ya malaria na kuanza kutumia lakini kichwa kiliendelea kuuma sana.

Alishia kusema anajuta kutokufuata ushauri wa daktari na hakika anajuta maana hata kutembea na uwezo wa kwenda kazini hana kwa sasa.

"Nina uhakika kama nilijua inaweza kuwa kwa namna hii, ningetumia dawa vizuri sana," alisema kwa masikitiko makubwa.

Kiharusi ni ugonjwa wa dharura ambao hutokea baada ya ubongo kukosa damu na kwa muda.

Ubongo wa binadamu unahitaji damu na okisijeni ili kufanya kazi zake za kila siku kisawia. Kama ikitokea ubongo umekosa kupata damu kwa mda mfupi mpaka muda mwingi, unaweza kuleta madhara makubwa kama kushindwa kutembea, kuongea na hata kufanya shughuli za kila siku.

Kiharusi kimekuwa moja ya changamoto kubwa zinazowakumba watu hasa wenye matatizo la shinikizo la damu, kuwa na tatizo la ugonjwa wa kisukari, tatizo la kuwa na lehemu (corestoral) nyingi katika mishipa yako ya damu ambayo huweza kusababisha kuziba kwa mishipa hiyo na kufanya ubongo kukosa damu na okisijeni. Kuvuta sigara husababisha kuharibika kwa mishipa ya damu ha hata pia kunywa pombe kwa kupitiliza.

**AINA ZA KIHARUSI**

Kuna aina mbili mpaka tatu za kiharusi, yaani kiharusi kinachosababishwa na damu kuvujia au kuvilia kwenye mishipa ya ubongo na damu kugandia kwenye mishipa ya ubongo. Pia kuna kiharusi cha kupita ambacho mtu anaweza kupata madhara ya muda tu ambayo huweza kurudi katika hali ya kawaida ndani ya saa 24.

Pamoja na kuwa na aina hizi za kiharusi zote bado huweza kuishia katika madhara makubwa kama yatajwayo hapo mwanzo, matababu yake huchukua muda mrefu sana na unahitaji watalamu tofauti tofauti ili kusaidia kupata haueni kidogo ya kutembea hata kuongea kwa kueleweka. Ni mara chache sana kurudi kuwa na hali uliyokuwa nayo mwanzo kabla ya kupata kiharusi.

Kwa hiyo matubabu yake inahitaji kada tofauti tofauti kama watu wa mazoezi ya viungo, mazoezi ya kuongea na matumizi ya dawa pia.

Ukweli ni kwamba tatizo la kiharusi linaweza kuzuilika kwa kuangalia afya yako, kufatilia na kufuata ushauri wa daktari, matumizi mazuri ya dawa za sukari, shinikizo la damu, kutokunywa pombe kupita kiasi au kuvuta sigara.

Ni vyema kukinga kuliko kutibu maana mwisho wa siku husababisha kuishia kwenye ulemavu wa kudumu na kupoteza nguvu kazi katika jamii hata familia kwa ujumla hasa pale anapopata mtu ambaye ni nguzo na mhimili mkuu kakika familia.

- **Dk. Budodi ni daktari wa magonjwa ya binadamu na anaishi Dar es Salaam. Kwa ushauri anapatikana kwa simu 0710 980096 na barua pepe mabulabudodi@gmail.com**



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Gracian Makota (kulia), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mwenza wa kampuni ya Chusa Mining Ltd, Damas Mwakipesile, kwa ajili ya kutambua mchango wa kampuni hiyo kwa kusaidia jamii inayozunguka migodi ya madini ya Tanzanite, katika mji mdogo wa Mirerani, jana. Wa (pili kulia) ni Mwenyekiti wa Chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Elisha Mnyawi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Bunge lataka utafiti mkanganyiko adhabu ya kiboko mbakaji miaka 18

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeipa jukumu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya utafiti wa kina kuhusu mkanganyiko wa sheria unaotoa adhabu ya viboko kwa kijana mwenye miaka 18 aliyetiwa hatiani kwa kosa la ubakaji kwa madai kuwa ni mtoto.

Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, aliyasema hayo juzi bungeni baada ya kuipa nafasi serikali kutafuta majibu sahihi kufuatia maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Agnesta Kaiza.

Katika maswali yake, Mbunge huyo alisema Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, inamtambua kijana wa miaka 18 kama mtu mzima, lakini katika sheria ya kupambana na masuala ya ubakaji, kijana wa miaka 18 anatambulika kama mtoto mdogo.

"Kijana huyu akienda kubaka, adhabu yake ni kupigwa viboko. Je, serikali haioni sheria hii imepitwa na wakati na hivyo kusababisha mgongano na Katiba mama?

"Na mko tayari kupitia upya sheria hii ili kuendana na wakati na kujulikana wazi kama kijana wa umri huo ni mtoto atakuwa hana sifa hizi zingine kama kupigakura, kuchaguliwa kuwa kiongozi na zinginezo?"alihoji

Hata hivyo, kutokana na swali hilo, Spika Tulia aliomba wabunge wabobezi wa sheria na serikali kujiridhisha kama kuna sheria inayotoa adhabu hiyo ili kutoa majibu sahihi kwa umma.

Kabla ya kumaliza kipindi cha maswali na majibu, Spika Dk. Tulia alitoa fursa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, kutoa ufafanuzi na alikiri uwapo wa adhabu hiyo.

Alisema Sheria ya Kanuni za Adhabu kifungu cha 131(2) imeweka angalizo kuwa kama makosa hayo yametendwa na mvulana ambaye ana umri chini ya miaka 18 na kama ni mara yake ya kwanza atapata adhabu ya viboko.

Johari alisema adhabu hiyo inakinzana na Sheria ya Mtoto kupitia kifungu cha nne ambacho kimetafsiri vizuri kwamba, mtoto ni yule ambaye yupo chini ya miaka 18.

Hata hivyo, alisema ofisi yake inalichukua suala hilo kwenda kuliangalia na kulifanyia utafiti ili kuona kama kuna haja ya sheria hiyo kuandikwa upya.

"Tutafanya utafiti kwanini tulikuja na suala hili la mtoto wa miaka 18 asifungwe kifungo cha maisha, ili tuweze kufanya maamuzi sahihi," alisema.

Kutokana na ufafanuzi huo, Spika Tulia, alisema Bunge limeiachia kazi ofisi hiyo kwenda kufanya utafiti kuhusu sheria hiyo.

"Tumewaachia mwende kufanyia kazi suala hili labda wakati wanatunga walikuwa na sababu na kama zimebadilika na kama kuna sababu ya hapa na pale basi tufanye marekebisho.

"Nakumbuka iliwahi kuletwa hoja kutoka Iringa, ililetwa na Mbunge Rose Tweve, kifungu hiki kilileta mgogoro yaani, mtu alikuwa ana miezi miwili ndio ametimiza miaka 18 halafu akabaka mtoto ikawa shughuli, inabidi aadhibiwe kama mtu mzima au kifungu hiki anakua nacho,"alisema.

Alisema kutokana na mkanganyiko wamewaachia wafanye utafiti ili kuwa na ulinzi wa watoto na kila mmoja alindwe na sheria hiyo.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge Agnesta alihoji kiwango gani sheria zilizopo za kupambana na matukio ya ubakaji zinajitosheleza.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, alisema Mwaka 1998, Bunge lilitunga aheria mahususi inayosimamia makosa ya kujamiiana na makosa yanayoendana nayo.

Alisema sheria hiyo ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; Sheria ya Ukomo wa Adhabu, Sura ya 90; na iliyokuwa Sheria ya Mtoto na Mtu mwenye Umri Mdogo, Sura ya 13.

"Lengo la kutungwa kwa sheria hiyo ilikuwa ni kumlinda mwanamke na mtoto dhidi ya makosa ya kujamiiana na makosa yote yanayoshabihiana. "Sheria hii iliongeza adhabu ya makosa hayo kuwa ni kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka 30 jela," alisema.

Alisema kwa kiasi kikubwa sheria zilizopo zinajitosheleza kupambana na matukio ya ubakaji.

# Rais Mwinyi asisitiza uwekezaji kukuza ajira

**Na Romana Mallya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kuimarisha sekta ya uwekezaji na shughuli za biashara ili kukuza uchumi na kuongeza fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Amesema tayari serikali imesajili na kutenga zaidi ya miradi 330 yenye thamani ya mtaji wa USD bilioni 5.4 ili kuzalisha ajira zaidi ya 18,000 kwa sekta mbalimbali zikiwamo, utalii yenye miradi 112, biashara ya majengo 56, viwanda 36 na sekta nyingine.

Dk. Mwinyi ambaye pia ni rais wa Zanzibar aliyasema hayo jana katika viwanja vya Gombani, Kaskazini Pemba, alipozindua Kampeni ya Kijana Kijani Pemba ikiwa ni shamrashamra za kupongeza miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane, anayoiongoza.

Alisema serikali imetoa vifaa vya uzalishaji kwa vijana vyenye thamani ya Sh. milioni 985.503 kwa vikundi 420 pamoja na ruzuku ya Sh. milioni 338.611 kwa vikundi 395 vya vijana ili kuwainua na kuwawesha kiuchumi.

Katika kuhakikisha wananchi wanapata mitaji ya kuendesha shughuli zao, Rais Dk. Mwinyi alisema, hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu, kupitia Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 31.8 kwa wajasiliamali wadogo wadogo Unguja na Pemba, ambapo asilimia 40 ya wanufaika ni vijana wa umri kati ya miaka 18- 35.

Rais Mwinyi pia alisema kujengwa kwa vituo vya wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kwa kila wilaya ni kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kwa kuwapa maeneo mazuri ya kufanya shughuli zao na kuzalisha fursa za ajira.

Akizungumzia nia ya serikali kuendeleza juhudi ya kuifungua Pemba kimaendeleo, Rais Mwinyi alisema serikali imeendeleza kazi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara kuu na za vijijini, kutengeneza bandari za mkoani na Shumba na kuanza matayarisho ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

Alisema serikali inaendelea kuimarisha eneo la uwekezaji la Micheweni na eneo la viwanda Chamanangwe kwa kuyawekea miundombinu na kuongeza kuwa, tayari kuna wawekezaji waliojitokeza kuwekeza maeneo hayo, hatua aliyoieleza kwamba, itaongeza fursa za ajira kwa vijana.

Akizungumzia kuhusu kuimarisha shughuli za biashara na ujasiriamali kwa vijana, Rais Mwinyi alisema mafanikio ya Serikali ya Awamu ya nane ya ujenzi wa masoko makubwa ya kisasa likiwamo Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini ambayo mawili tayari yashafunguliwa.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema wananchi wa Pemba wanafahamu thamani ya maendeleo na kuona juhudi za Rais Mwinyi na Wanzanzibar wanaupenda uongozi wa serikali.

Aliwasihi wananchi wa Zanzibar kujihusisha na siasa ni maendeleo sio ugomvi.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, UVCCM na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Joketi Mwegelo, alisema CCM itashinda kwa ushawishi na imani kubwa kwa viongozi wao.

Alisema CCM hakiyumbishwi kwa chokochoko na majungu ya uvunjifu wa amani, bali misimamo ya viongozi wa kuu wa nchi wanaohubiri na kusisitiza umoja, utulivu, msikamamo na uthubutu.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Masoud, akiwawakilisha wananchi wa mikoa miwili ya Pemba Kusini na Kaskazini, alipongeza juhudi kubwa ya maendeleo iliyofanywa ndani ya kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Mwinyi.

Pia alisifu hatua ya serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kujenga madarasa 661 kwa mikoa yote ya Pemba skuli za ghorofa 13, ajira za walimu 1,500 kutolewa vibali vya ajira za walimu, 600 ujenzi wa vyoo 953 kwa skuli mbalimbali na ujenzi wa hospitali kwa wilaya tatu za Pemb.

Kadhalika ukarabati mkubwa kwa hospitali ya Abdalla Mzee, kuongezwa kwa chumba cha ICU na uchunguzi na ajira 468 sekta ya afya na huduma nyingine za jamii.

# MAISHA

NOVEMBA 3, 2024

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

Jumapili




## HARUSI

Ukurasa 12





# MAKOSA WAKATI WA KUJIPODOA

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | ■ | M | A | M | B | O |
| J | ■ | ■ | ■ | W | ■ | N |
| A | ■ | B | A | A | ■ | G |
| R | A | I | ■ | K | O | O |
| I | ■ | S | A | A | ■ | P |
| B | ■ | H | ■ | ■ | ■ | E |
| U | K | A | M | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


TAA, MEI, LOA, OTA, SHARI, EBOLA, ASALI, TAMKO, MABONDE, ICHACHE

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HAYA, KILA MMOJA MFIKISHE KATIKA JINA LAKE.





## PAKA RANGI



@Msamba

## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Unajua hatari ya ndoto unazoota usiku?

KARIBU tena msomaji wangu tumulike maisha yetu yalivyo kila uchao. Leo nijadili kidogo kuhusu hatari ya ndoto unazoota ukiwa umelala. Ulimwengu wa ndoto unaelezewa kuwa ni muhimu kama ulivyo ulimwengu wa damu ya nyama.

Je, unajua mwanadamu ni matokeo ya ndoto anazoiota? Ndoto ni njia mojawapo ya mawasiliano. Ni hatari kupuuzia ndoto unazoota kwani ndoto ni picha ya maisha yako kwenye ulimwengu wa roho, ambao hauonekani kwa macho.

Ndoto hazidanganyi. Unaweza kushindwa kuielewa ndoto unayoiota lakini ndoto haidanganyi. Ndoto huonyesha maisha yako ya mbele na ya nyuma.

Kila ndoto unayoiota hubeba ujumbe hata kama huelewi kwa wakati huo, maana shetani anapenda sana kufuatilia maisha ya ndoto ya mwanadamu na kupenyeza uovu wake. Upo wakati hujigeuza malaika wa nuru na kuwadanganya watu kupitia ndoto.

Shetani anajua kuwa akishafanikiwa tu kutawala maisha yako ya ndoto anaweza kuharibu na kupindisha hatma yako bila kipingamizi ndio maana hupaswi kabisa kupuuza ndoto unazoota. Mungu naye hutumia ndoto kama njia ya kuokoa watu wake na kuwakingia na hatari.

Msomaji wangu hebu sasa tuangalie nini maana ya ndoto. Zipo maana nyingi zinazoelezea ndoto lakini hebu nikupitishe katika baadhi ya maana za ndoto.

Ndoto ni taarifa unayopewa kwa njia ya pich ukiwa umelala. Iwe ni ndoto imetoka kwa Mungu au kwa shetani lazima utaona picha. Kwa mfano, taarifa ya habari hueleweka Zaidi pale unapoiona kwenye luninga kuliko kusikia tu.

Ndoto ni mlango unaokupeleka kwenye ulimwengu wa roho. Ndoto ni kitu halisi kinachoendelea kwenye maisha yako katika ulimwengu wa roho. Kumbuka mwanadamu ni roho yenye nafsi inayokaa kwenye mwili!

Pia ndoto ni unabii wa mambo yatakayokuja kutokea kwenye maisha yako. Ndoto huonyesha wapi ulipofungwa kwenye ulimwengu wa roho. Ndoto hufunua siri zilizojificha.

Ndoto zina nguvu ya kufungua milango iliyofungwa kwenye ulimwengu war oho maana humwonyesha mtu jambo na maombi gani ya kufanya ili kuifanya hiyo ndoto iwe kitu halisi.

Ndoto ni njia rahisi ambayo Mungu anaongea na mwanadamu. Kwenye ndoto Mungu huongea na mtu yoyote, iwe mkristo au mpagani.

Mungu huongea na mpagani ili kumuonya na kumvuta kwenye wokovu. Mungu huongea na wanadamu kuwafundisha, kuwaelekeza, kuwaonya na kadhalika. Ndoto haikuonyeshi tu mambo mema au mabaya bali huleta maonyo mbalimbali kwetu.

"Katika ndoto, katika maono ya usiku, usingizi mzito uwajiliapo watu, katika usingizi kitandani; ndipo huyafunua masikio ya watu, na kuyatia mhuri mafundisho yao, ili amwondoe mtu katika makusudio yake, na kumfichia mtu kiburi; yeye huzuia nafsi yake isiende shimoni, na uhai wake usiangamie kwa upanga"(Ayubu 33:15-18).

Msomaji wangu, ni muhimu uelewe ndoto unazoota kwani wengi kwa kushindwa kupata tafsiri halisi ya ndoto walizoziota walipata madhara makubwa. Wengi wamekufa baada ya kuota ndoto, wengi waliharibikiwa baada ya kuota ndoto. Wengine walianza kushambuliwa na maradhi baada ya kuota ndoto!

Sasa hebu tuone aina za ndoto. Kwanza ni ndoto kutoka kwa Mungu. Pili ndoto kutoka kwa shetani na wajumbe wake. Tatu, ndoto kutokana na shughuli za kila siku na ndoto kutokana na kuugua muda mrefu.

**"Ndoto hazidanganyi. Unaweza kushindwa kuielewa ndoto unayoiota lakini ndoto haidanganyi. Ndoto huonyesha maisha yako ya mbele na ya nyuma.**

Ndoto zimegawanyika katika makundi sita. Ndoto zinazoongeza kitu kwenye maisha yako. Mfano unapoota mtu anakukabidhi kitu kizuri kwenye ndoto, na unapoamka unashangaa unapandishwa cheo kazini au maisha yako yanaanza kubadilika na kuwa mazuri, ujue hiyo ndoto imekuongezea kitu kwenye maisha yako!

Ndoto zinazopunguza kitu kwenye maisha yako. Mfano, mjamzito analala na kuota anazini kwenye ndoto na akiamka asubuhi anakuta mimba imeharibika. Ujue hiyo ndoto imepunguza kitu kwenye maisha yako.

Ndoto zinazokuacha ulivyo bila kukudhuru. Mfano, unafanya kazi benki na usiku unaota unahesabu fedha, au wewe ni mfanyibashara na unaota unauza bidhaa kwenye duka lako.

Ndoto zinazokufanya uishiwe kila ulicho nacho. Mtu mmoja aliota amepoteza fedha, baada ya siku chache alifukuzwa kazi na kunyang'anywa kila kitu alichopewa na kampuni. Kila alichoanzisha baada ya hapo kilikufa, chanzo kilikuwa ni ndoto. Wiki ijayo sababu za kuota!

***Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Ujumbe mfupi 0715268581. Namba hii ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Bajeti ya familia ni kitanzi kwa wanaume?

BAJETI ya familia ni mpango wa fedha unaosaidia familia kupanga matumizi yao ya kila mwezi au mwaka.

Bajeti ya familia ni ile inayojumuisha mapato yote ya familia kama mishahara na matumizi mbalimbali ya chakula, kodi ya pango, huduma za afya na elimu.

Kwa nini bajeti ya familia? Lengo ni kuhakikisha familia inatumia fedha zake kwa ufanisi na inajikinga na matatizo ya kifedha.

Je, uwazi wa mapato na matumizi katika familia, unaweza kuimarisha uhusiano wa familia na kupunguza ukatili dhidi ya wanawake na watoto nyumbani?

Uwezekano ni mkubwa sana, hasa mtu anapokuwa na uhakika wa vyanzo vya mapato na matumuzi yake.

Kwa mfano, kukiwa na uwazi kuna kujenga imani na kuaminiana katika kuweka mipango ya pamoja, kutekeleza, kufuatilia na kuchambua mafanikio hayo tofauti na zile familia ambazo baba ana vyake na mama ana vyake.

Nilifundishwa hivi, kukiwa na bajeti ya familia, mmoja wa wanandoa na walioko katika uhusiano, hawawezi kuja kujenga maisha ya wasiwasi kwamba mwenzangu ana kipato zaidi yangu.

Wakati mwingine, bajeti ya familia inaepusha manung'uniko au lawama kwamba mimi sijui mapato yake yanaenda wapi.

Hili jambo mara nyingi ndilo limekuwa chimbuko la kuleta hatari ya kuchochea ukatili kwa sababu baba haamini au mama haamini kile kinachopatikana.

Tunachokiona ni kwamba hali hiyo ikitokea kuna hali ya sintofahamu ambayo kila mtu sasa hujaribu kuchunguza au kususia kile alichonacho na hivyo kumfanya mwingine kuonekana kwamba ni tegemezi au hajui kinachoendelea. Kibaya zaidi, mwingine anaweza akanyimwa asitoke tena kwenda kufanya kazi.

Mfano mzuri, mume anaweza kumzuia mke kufanya kazi au kufuatilia kila aina ya chanzo cha mapato alicho nacho au kufanya hata kazi ya kudokoa/ kuiba kile kipato kidogo ambacho mama anakuja nacho nyumbani.

Inapotokea hivyo, basi unakuta migogoro ya kifamilia ipo na baba anaanza kuitelekeza familia, akijua mama ana chake.

Kesi nyingi nilizokutana nazo nimejifunza kwamba wakati mwingine unakuta mwanamume hazingatii tena ule wajibu wake kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1970.

Sheria inatamka kwamba mume ana jukumu la msingi la kutunza familia. Hii ndiyo sababu kubwa inayochochea kukua kwa ukatili wa kiuchumi. Changamoto nyingi zinaweza kujitokeza kama familia haina bajeti.

Mosi, kukosekana kwa usawa wa fedha. Mmoja wa wanandoa anaweza kumnyonya mwenzake kipato chake na jambo hili linaweza kusababisha matumizi kupita kiasi.

Pili, mizozo ya kifamilia. Kutokuelewana kuhusu matumizi ya vipaumbele kunaweza kuvuruga amani ya familia na kuwapo migogoro ya mara kwa mara.

Tatu, familia inakosa kuwa na akiba ya fedha. Kwamba ikitokea mtoto au mama ameugua ghafla, familia inaweza kushindwa kwa dharura kama ugonjwa na ajali.

Nne, familia kukosa malengo ya fedha. Familia inaweza kukosa malengo ya muda mrefu kama kununua kiwanja cha makazi au kugharamia ada za watoto shuleni.

Tano, kushindwa kushiriki ipasavyo shughuli za kijamii. Familia nyingi zinakosa fefha za kushiriki katika matukio ya kijamii au shughuli za kijamii.


Kuwa na bajeti, ni muhimu katika kudumisha utulivu wa kifedha au kujiandaa kwa mahitaji ya baadae.

**• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

**"Sheria inatamka kwamba mume ana jukumu la msingi la kutunza familia. Hii ndiyo sababu kubwa inayochochea kukua kwa ukatili wa kiuchumi. Changamoto nyingi zinaweza kujitokeza kama familia haina bajeti.**



Oktoba 6, mwaka huu ilikuwa siku ya furaha kwa Nyamisi Kasika wakati alipofunga ndoa na Isack Yona katika Kanisa la Sabato la Mbezi Luis mkoani Dar es Salaam. Sherehe ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Tunu. Mungu awape maisha marefu yenye furaha na upendo. **PICHA: SABATO KASIKA**







# MITINDO

Na Moshi Lusonzo







## JIPENDELEE UKIWA NA VESTI

VESTI ya nailoni iliyojazwa pamba nene ni vazi lina mwonekano wa kuvutia pale linapovaliwa nyakati za baridi.

Vazi hili linapendeza zaidi kuvaliwa na wanaume linahifadhi joto la kiasi na hivyo kumpa mvaaji furaha zaidi.

Kitambaa kilichounganishwa ndani kinatoa nafasi ya mwili kupumua, ni laini, na inanyonya unyevu ili kukusaidia kuwa mkavu kwa siku nzima.

Vesti ya aina hii imetengenezwa kwa nailoni ya 380T yenye uwezo wa kuzuia maji.

Kizuri zaidi inaweza kukabiliana na mvua kidogo au ukungu, kukupatia joto na ukavu unapokumbana na mvua nyepesi ya ghafla wakati unapotembea kwa miguu au pikipiki.


Itapendeza zaidi kama ndani utavaa shati jepesi ambalo halitazidisha joto na kukupatia kero.

Chini inakupa machaguo mengi kwani inapendeza kwa suruali ya kitambaa, jeans na kaptura ya aina yoyote.

Kuhusu viatu, wengi wanapendelea kutoka na buti, raba au viatu vya kutumbukiza.

UREMBO

# Makosa wakati wa kujipodoa



IMEZOELEKA kwa wanawake duniani kote kutumia vipodozi kama njia ya kujiongeza uzuri wao wa asili.

Hata hivyo, kuna baadhi ya makosa yanafanyika wakati wa kujipodoa na kusababisha kupoteza maana nzima ya kijremba na kuonekana kituko.

**Kukwangua nyusi zote**

Kuna baadhi ya wanawake wananyoa nyusi zao usoni na kuzitoa kabisa. Halafu, wanaishia kuzichora na rangi nyeusi.

Hii inamfanya mwanamke kuonekana kama kituko.

Unatakiwa kupunguza kwa kiasi kidogo, usitumie rangi nyeusi kuzijaza. Tumia rangi ya brauni na kwa mwonekano wa kiasili zaidi, tumia nyusi, poda ya nyusi au mafuta badala ya penseli.

Usitumie foundesheni

Kupata foundesheni inayofanana na ngozi yako ni ngumu, hasa kwa wanawake wenye ngozi nyeusi tii.

Wanawake wengi wanapata shida na kukubali rangi ya kiasili na wanajaribu kutumia vipodozi kubadilisha rangi yao.

Kama hakuna foundesheni inayofanana na rangi yako, basi kubali kwani ukilazimisha kujipaka unaweza ukawa mweusi au mweupe zaidi kutegemea na rangi yako.

Kwa hiyo ni bora kuwa na faundesheni inayoendana na mabadiliko hayo.

**Punguza poda**

Wanawake wengi wanafikiri kwamba kutumia poda nyingi ndio kupendeza zaidi. Matokeo yake, wanaishia kukosa mvuto.

Tumia poda inayofanana na ngozi yako usiweke poda nyingi. Kiasi kidogo kitakutosha na tumia brashi kujisugua.

Hakikisha unatumia brush kwenye mifupa ya mashavu, sio kwenye mashavu yenyewe.

Kama una ngozi yenye uweusi zaidi, tumia blush ya rangi ya dhahabu au zambarau.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Maandazi ya kuoka

MAANDAZI ya kuoka ni aina ya vitafunwa vinavyopikwa bila kukaangwa kwa kutumia mafuta.

Kwa wale ambao wamezuiwa kula vyakula vya mafuta, mlo huu ni rafiki na rahisi kupika.

**Mahitaji**

Unga wa ngano nusu, sukari kikombe kidogo kimoja, hiliki punje 10, samli kijiko kimoja cha chakula, Tui la nazi glasi ndogo moja na hamira pakiti moja.

**Maandalizi**

Chekecha unga kwa kutumia chujio kwenye chombo utachokandia unga wako, kisha punguza unga nusu kikombe weka pembeni.

Chukua kikombe kingine weka hamira, sukari kijiko kimoja, unga kijiko kimoja na tui vijiko vitatu iache kwa dakika tatu mpaka ifure.

Twanga hiliki zilizomenywa kisha weka kwenye unga unaotaka kuukanda

Chukua unga ulio uweka hiliki, weka sukari na samli halafu changanya kwa mkono vizuri.

Chukua hamira iliyoumuka changanya kwa kutumia mkono vizuri.

Malizia kwa kumimina tui lako kidogo kidogo na uanze kuukanda hadi utakapo kuwa donge moja.

Kanda unga kwa dakika 10 mpaka uwe mlaini kisha ufunike vizuri au uweke kwenye container na uufunike ili usipitishe hewa uache kwa dakika 5 kwenye sehemu ya joto.

Ukiumuka kata madonge na uyasukume kwa kutumia unga mkavu ili upate duara.

Hata hivyo lisiwe nene sana wala jembamba sana kisha kata maandazi yako kwa shape ya pembe tatu.

Weka unga mkavu kwenye tray na ueneze kisha panga maandazi unayotaka kuoka

Yaache maandazi yako yaumuke kwa dakika zisizo pungua 20.

**Jinsi ya kupika**

Washa Oven moto wa juu na chini nyuzi joto 140, oka maandazi yako kwa muda wa dakika 20, yakianza kuweka rangi ya dhahabu yatoe.

Weka kwenye sahani na tayari kwa kula ikiwa na maharage, mboga, mchuzi, chai au kinywaji chochote.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Tumia ubunifu kurembesha 'dressing room'

SEHEMU ya chumba kinachotumika kuvalia nguo (dressing room) ambacho pia wengi hutumia pia kupumzika, ni muhimu na ndipo mahali pekee ambapo huchangia kumtoa mtu akiwa amependeza au amechukiza.

Watu wengi wanaokuwa wamependeza wanapotoka ndani na kuvutia machoni mwa watu ikiwamo kusifiwa kwamba wamependeza, siri yake huwa ni chumba maalum ambacho hutumika kuvalia.

Kutokana na umuhimu wake, kuna haja kubwa ya kuhakikisha kinawekwa katika mazingira mazuri na ya kuvutia kama ambavyo watu wanaokitumia hutoka humo wakiwa wamependeza na kusifiwa na watu na kujiona 'babkubwa'.

Fahamu kwamba kabla ya kupangilia chochote katika chumba hiki, kitu cha kwanza kabisa ni kitanda kikifuatiwa na vitu vingine.

Leo nimeona nizungumzie namna ya kupangilia chumba hiki katika mtindo na kama sehemu pia inayotumika kwa ajili ya kuvalia.

Mbali na kitanda kuwekwa na mpangilio wake maalumu, lazima tuhakikishe kwamba vitu vingine vinavyokipamba navyo vinawekwa katika utaratibu mzuri unaoeleweka na si tu kuweka kama pango la wanyang`anyi.

Vitu vya muhimu vya kuzingatiwa vya kusaidia kupamba chumba hiki na kithaminike kuwa kinasaidia kumtoa mtu akiwa amependeza ni pamoja na kuhakikisha kupangilia vifaa vyote katika eneo lake vinavyowekwa kwenye chumba chako hicho.

Miongoni mwa vinavyotakiwa kupangiliwa vizuri katika chumba hiki ni kabati la nguo kwa sababu ndilo hutumika katika kuhifadhia nguo na pia unapokuwa nalo linasaidia kupunguza mlundikano hovyo wa nguo ambao unaweza kuwapo.

Hakikisha kabati lako linawekwa sehemu ambayo ni sahihi, kama ni la ukutani au la kusimamisha kawaida, hakikisha linawekwa sehemu sahihi ambalo pia haliwezi kufinya nafasi ya kuwekwa kitu kingine.

Katika mpangilio wa kabati unapaswa kuangalia sehemu sahihi ya kuliweka, aidha liwe la ukutani au la kusimama kawaida.

Kitu cha pili ni kuangalia namna ya kupangilia 'dressing table' yako, hapo pia unapaswa kuwa mbunifu kwa kuangalia eneo sahihi ambalo pia itakuwa rahisi kwa matumizi yako.

Kingine ni mpangilio wa pochi, hizi nazo zinapaswa kutundikwa katika stendi yake maalum katika eneo lake maalumu.

Mpangilio wa viatu ni jambo lingine muhimu. Hivi navyo vinatakiwa viwekwe katika mpangilio mzuri ili visiharibu muonekano wa chumba.

Ikiwezekana hakikisha unaandaa fremu maalum kwa ajili ya viatu tu na ikiwezekana vipangiliwe kulingana na muundo wake ili kuongeza mvuto, kama ni virefu viwekwe kwa mpangilio wake na vifupi hivyo hivyo.

Jambo ninalotaka kusisitiza hapa ni kwamba si vibaya kama kila kitu kinachowekwa katika chumba hiki kinazingatia rangi za vitu vilivyopo katika chumba hicho, kwa sababu hii ni nyezno muhimu katika kunogesha chumba.





# Usitumie kemikali bustanini

Na Restuta James

ZAMANI, wazee walijua jinsi ya kutumia mimea asilia ili kuzuia wadudu waharibifu wa mazao na afya ya binadamu, kama mbu na minyoo ya udongo.

Njia hizi ambazo ni rafiki mkubwa wa mazingira kwa kuwa hazihusishi matumizi ya kemikali, zilifanikisha kufukuza nzi na visumbufu vingine kwenye mazao hasa matunda na mboga mboga, zinapendekezwa na wataalamu hasa kwa wapenda bustani.

Watafiti wa masuala ya mimea wanaeleza kuwa mimea mbadala inaweza kupandwa kama kiuatilifu kwenye bustani ya maua au mboga.

Pamoja na kuwapo kwa dawa za kuua mbu, viatilifu vya kukabili visumbufu vya matunda na mboga, mbinu za kale ni bora na salama zaidi, kwa kuwa zinaepusha matumizi ya kemikali zinazoharibu mazingira.

Unaweza kuzuia mbu, mende na wadudu wengine warukao, kwa kupanda aina aina hii ya maua katikati ya bustani yako ya maua, mbogamboga na matunda.

Kwanza kabisa, maua haya ambayo unaweza kusema ni viuatilifu, yanasaidia katika uchavushaji, kuvutia wadudu wenye faida kama nyuki na kuongeza tija ya mazao.



BORAGE

Borage au uanyota ni mlinzi mkubwa wa zao la nyanya kwa wale wanaozingatia kilimo hai, hasa bustani kwa matumizi ya nyumbani. Linazuia minyoo ya nyanya, ya kabichi na huvutia nyuki.

MARIGOLD

Hili ni ua muhimu kwa ajili ya kuipa furaha na afya mimea mingine bustanini.

Inazuia wadudu waharibifu kwenye mboga kama nyanya, kabichi, brokoli na cauliflower.


Kwa ujumla, mimea hii inavumilia jua na inachanua kipindi chote cha mwaka. Inaweza kupandwa kwenye makopo au chini, kulingana na matumizi ya mhusika au eneo. **0753333330**

# KATUNI

## KATUNIKA KI'DOMOKRASIA


BY ABDUL KINGO - 2024

SMS - 0713 447766




## JUKWAANI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

HABARI KIMATAIFA

# Rais Ukraine aomba msaada kukabiliana na Korea Kaskazini

**KYIV,** UKRANE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, ametoa wito kwa mataifa ya Ulaya na Marekani kuacha kutazama kinachoendelea nchini mwake, bali wachukue hatua kwa kukabiliana na uwepo wa wanajeshi wa Korea Kaskazini nchini Russia.

Katika hotuba yake, Rais huyo alisema Korea Kaskazini imepata maendeleo katika uwezo wake wa kijeshi, utengenezaji wa makombora na silaha, hivi sasa wanajeshi wake wanapata mafunzo yatakayowawezesha kushiriki kwenye vita nchini humo wakiisaidia Russia.

Kiongozi huyo alisema nchi yake imebaini eneo walilopo wanajeshi wa Korea Kaskazini lakini hawawezi kuwashambulia kwa sababu washirika wake wa magharibi hawajatoa silaha za masafa marefu ambazo wangezitumia kuwashambulia wanajeshi hao.

Wiki hii Marekani ilisema kuna wanajeshi 10,000 wa Korea Kaskazini nchini Russia wakiwemo 8,000 katika eneo la Kursk.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Korea Kaskazini, Choe Son Hui, alimuhakikishia kiongozi mwenzake wa Russia, Sergei Lavrov kuwa nchi yake itasimama hadi pale itakaposhinda vita vyake dhidi ya Ukraine.

**DW**

# Watu 50,000 wapata chanjo homa MPox DRC, Rwanda

**KINSHASA,** DRC

ZAIDI ya watu 50,000 wamepatiwa chanjo ya virusi vya homa ya mpox katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Rwanda.

Katika taarifa ya Shirika la Afya Ulimwenguni, ilisema mlipuko huo bado haujadhibitiwa.

Hata hivyo, shirika la afya la Umoja wa Afrika, limeonya na kutoa wito kwa kupatikana kwa rasilimali zaidi ili kuepuka janga hilo kuwa kubwa kuliko usambaaji wa virusi vya Uviko 19 la miaka michache iliyopita.

Kwa mujibu wa ripoti ya Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa Afrika (CDC), zaidi ya watu 1,100 wamekufa kwa ugonjwa wa mpox barani Afrika, na 48,000 wameorodheshwa kuambukizwa tangu Januari mwaka huu.

DRC ndio nchi iliyoathirika zaidi na ugonjwa huo na inaongoza kwa idadi ya watu waliokufa.

**DW**

# Hali mbaya Mashariki ya Kati, Marekani yapeleka jeshi lake

**WASHINGTON,** MAREKANI

HALI inazidi kuwa mbaya eneo la Mashariki ya Kati baada ya Israel kuendelea kushambulia maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Gaza na Lebanon.

Jana mashambulizi ya anga yalisababisha vifo vya Wapalestina kadhaa baada ya kulenga kambi ya wakimbizi ya Nuseirat katika mji wa Jabalia ulioko kaskazini mwa Ukanda wa Gaza.

Vyanzo vya habari vya Palestina vilisema kuwa jeshi la anga la Israel lilishambulia shule ya Al-Rafei, ambayo inawahifadhi wakimbizi waliokimbia makazi yao katika mji wa Jabalia na kuwaua Wapalestina kadhaa.

Wapalestina watatu, wakiwemo watoto wawili, pia waliuawa katika shambulio la bomu lililolenga nyumba moja katika kambi hiyo.

Wapalestina watano wamejeruhiwa katika mashambulizi hayo mapya ya makombora.

Vikosi vya Israel vimeendelea kushambulia Ukanda wa Gaza tangu Oktoba 7, 2023 na kuwaua zaidi ya Wapalestina 43,000 na kuwajeruhi wengine 102,000.

Wakati huo huo, Wizara ya ulinzi ya Marekani, ilisema jana kuwa imeagiza kupelekwa kwa makombora ya ziada ya masafa marefu, vikosi vya wapiganaji, ndege za mafuta na makombora kadhaa za masafa marefu katika eneo la Mashariki ya Kati.

"Kwa mujibu wa ahadi zetu za kuwalinda raia wa Marekani na vikosi vya Mashariki ya Kati, kuilinda Israel, na kupunguza mvutano kupitia kujizuia na diplomasia, Waziri wa Ulinzi ameamuru kupelekwa kwa makombora ya ziada ya masafa marefu, kikosi cha wapiganaji, na ndege kadhaa za kivita za Marekani aina ya B-52 za masafa marefu katika eneo hilo," ilisema taarifa ya Pentagon.

Taarifa hiyo iliongeza"Vikosi hivi vitaanza kuwasili katika miezi ijayo wakati kundi la mashambulizi la USS Abraham Lincoln likijiandaa kuondoka."

Pia aliongeza kuwa kupelekwa kwa makombora hayo kunatokana na uamuzi wa hivi karibuni wa kupeleka mfumo wa ulinzi wa makombora wa Terminal High Altitude Area Defense (THAAD) nchini Israel pamoja na msimamo unaoendelea wa kitengo cha ulinzi cha Jeshi la majini katika Mashariki mwa Mediterranean.

**BBC**




Raia wa DRC wakipatiwa chanjo ya ugonjwa wa Mpox hivi karibuni. **PICHA: DW**

# Niger yapinga kufungwa mgodi wake wa uranium

**NIAMEY,** NIGER

NIGER imepinga uamuzi wa kampuni ya Orano ya kusimamisha uzalishaji wake wa madini ya uranium nchini humo.

Kampuni hiyo yenye makazi yake nchini Ufaransa ilitoa tangazo la kusimamisha uzalishaji wiki moja iliyopita.

Serikali ya Niger, ni mwanahisa mwenza wa kampuni ya Somair, ilisema usitishaji wa mgodi wa mwisho uliokuwa ukishughulikiwa na kampuni ya Orano nchini Niger, inatangaza kuwahusisha pande zote mbili.

Aidha, serikali ya kijeshi ya Niger ilieleza masikitiko yake kupitia taarifa iliyotolewa juzi.

"Licha ya hadhi yake kama mwanahisa mwenza, Sopamin haikushauriwa kuhusu uamuzi huu mzito." Ilisema taarifa hiyo

Kampuni ya HYPERLINK "https://www.rfi.fr/sw/lebo/ufaransa/" \t "_self" Ufaransa ya Orano, ambayo ina hisa nyingi katika kampuni ya Somair, ilitangaza siku nane zilizopita kwamba itasitisha uzalishaji wake wa uranium kwenye eneo hilo la mwisho kufanya kazi nchini Niger.

Sopamin ilishutumu ukosefu wa uwazi kutoka kwa kampuni hiyo ya Ufaransa, pamoja na ukiukaji wa kanuni.

Orano, kwa upande wake, ilitaja kuongezeka kwa matatizo yake ya kifedha, yanayohusiana na kuondolewa kwa kibali chake kwenye amana ya Imouraren na kutowezekana kwa usafirishaji wa uranium.

Pia ilisema mgogoro wa mpaka kati ya Niger na Benin unaongeza ugumu wa usafirishaji wa Uraniam.

Aidha, mapendekezo yake ya kusafirisha uranium kwa njia ya anga kwenda Ufaransa na Namibia yalikataliwa na serikali.

Katika kuinusuru Somair isisitishe shughuli zake, Niger ilisema itanunua tani 210 za uranium kati ya 1000 zilizozuiwa.

**RFI**

# Tembo waharibifu wadhibitiwa kwa dawa yenye harufu mbaya

**Na Ashton Balaigwa,** LIWALE

TEKNOLOJIA ya Kutengeneza Uzio wa Harufu Mbaya waliofundishwa wananchi wa Vijiji 11 katika Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, katika Pori la Akiba la Selous umesaidia kufukuza tembo wanaofanya uharibifu wa mazao katika mashamba na hivyo, kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori.

Ofisa ujirani mwema kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Kituo cha Selous Liwale, Aloyce Assenga, alisema migangano hiyo imeanza kupungua kupitia uzito huo wa harafu mbaya kuwa kero kwa tembo.

Alisema dawa hiyo iliyotoa matokeo chanya katika vijiji hivyo 11, imetengenezwa kupitia Mradi Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), ambaye ni mdau mkubwa wa TAWA.

"Baada ya kutengeneza harufu mbaya katika uzio tuliendа kwaajili ya kupata mrejesho, jamii imeonesha waziwazi mapokeo chanya kuwa inasaidia kufukuza wanyama wakali hasa tembo katika mashamba," alisema.

Assenga ambaye pia ni Ofisa Mhifadhi Wanyama Daraja la Kwanza, alisema kupitia mashirikiano baina ya TAWA na Mradi wa Shirika la GIZ, wametoa ufadhili wa mafunzo kwa Askari Wanyamapori wa Vijiji (VGS) ili kusaidiana na wale wa TAWA kwaajili kudhibiti wanyama hao kuingia mashambani.

"Kazi hii ya hatufanyi peke yetu kama TAWA, tunashirikiana na askari hao ambao wamepewa mafunzo kupitia ufadhili wa Shirika la GIZ, ambao walipatiwa elimu namna ya kusaidiana na askari kutoka TAWA wanaokaa katika vituo vyetu," alisema Assenga.

Alisema askari hao wanapatiwa vifaa mbalimbali yakiwamo mabomu, tochi na pikipiki ambazo husaidia kkufika kwa haraka katika maeneo ambayo yameripotiwa wanyama waharibifu.

Ofisa Kilimo anayeshughulikia Mradi wa GIZ, katika Wilaya ya Liwale, Anthony Kawishe, alisema kutokana na kuwapo kwa changamoto kubwa ya uvamizi wa tembo, GIZ wamekuja na mradi wa kukabilina na migongano kati ya binadamu na wanyamapori.

Alisema kutokana na tatizo hilo, Shirika la GIZ walitoa mafunzo kwa maofisa ugani wa vijiji 11 vya mradi wa namna ya kutengeneza harufu mbaya ya uzio ambao nao walitoa mafunzo hayo kwa wananchi wa vijiji vyao.

"Baada ya mafunzo hayoi kilitengeneza mbinu hiyo ya harufu mbaya ya uzio na kuwekwa mashambani na kusaidia maeneo mbalimbali ikiwamo yale ya wakulima wanaolima mpunga ambayo tembo waliondoka," alisema.

Ofisa Ugani wa Kijiji cha Turuki, Kata ya Mihumo, Tarafa ya Liwale Mjini, wilayani Liwale, Yunufu Luwongo, alisema GIZ wameweza kutoa mafunzo kwa vijana watatu kwenda katika mafunzo ya askari wanyamapori wa vijiji kwaajili ya kudhibiti wanyama waharibifu na tayari, wamehitimu na kuanza kazi hiyo katika kijiji hicho.

# SMZ yaongeza bajeti ya elimu

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

SERIKALI ya Mapindizi ya Zanzibar imesema imeongeza bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutoka Sh. bilioni 83.2 mwaka 2021/22 hadi Sh. bilioni 518 mwaka 2024/25.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (pichani), alisenma hayo juzi alipofungua skuli mpya ya ghorofa tatu ya Sekondari ya Konde, Micheweni, Pemba ikiwa ni mwendelezo wa kupongeza miaka minne ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya nane anayoiongoza.

Alisema bajeti hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 522.6 ambayo imesaidia kufanikisha utekelezaji wa miradi mingi ya kimkakati inayolenga kuimarisha elimu na kuweka misingi imara ya maendeleo ya muda mrefu ya taifa.

Kuhusu bajeti ya elimu ya juu, Rais Dk. Mwinyi alisema serikali imeongeza mikopo ya elimu ya juu kutoka Sh. bilioni 11.5 kwa mwaka 2021/22 hadi bilioni 33.4 mwaka 2024/25 ambayo imeongeza idadi ya wanafunzi kutoka 4,289 hadi 6,060.

Dk. Mwinyi alisema hadi sasa serikali tayari imejenga madarasa 2,773 sawa na asilimia 184 ya shabaha ya madarasa 1,500 yaliyoelekezwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, yenye uwezo wa kuchukua wastani wa wanafunzi 45 kwa shifti moja.

Alisema ujenzi huo pia umejumuisha ukamilishaji wa madarasa yaliyoanzishwa na wananchi, ujenzi wa madarasa mapya, pamoja na shule 53 za chini na 26 za ghorofa.

Pia alisema mafanikio hayo yanajumuisha ujenzi wa shule 35 za ghorofa katika maeneo mbalimbali na kwa mkoa wa Kaskazini Pemba, tayari ujenzi wa shule za ghorofa sita umekamilika.



Akizungumzia hatua ya ujenzi wa madarasa mapya 2,037, Rais Dk. Mwinyi alisema kazi hiyo inaendelea na tayari serikali imeajiri walimu 3,531 pia imejenga maabara za Fizikia, Kemia na Baiolojia katika kuimarisha mitaala ya sayansi.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema ufunguzi wa shule mpya ya sekondari Konde ni fursa adhimu kwa wananchi wa eneo hilo, hivyo aliwasihi wananchi wa Zanzibar kuendelea kumuunga mkono Rais Dk. Mwinyi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdalla Said, alisema Shule ya Sekondari Konde ina uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,890 na wastani wa wanafunzi 45 kwa darasa moja kwa wakati mmoja.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alipongeza juhudi za maendeleo zinazofanywa na serikali ya awamu ya nane kwa kutimiza mambo ya msingi kwa wananchi.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Usiwe 'kidomidomi' kwenye mapenzi ya watu



**Na Adam Fungamwango**

> **"Yaani ukimkubali nitakuona wewe hamna kitu kabisa shoga yangu, mkubali fulani, yule ana pesa, anakupenda na anakujali." Atampigia debe mwanaume mwingine ambaye labda humpa pesa kwa ajili ya kulaisha**

MAPENZI ni ridhaa ya mtu mwenyewe kutamani au kumpenda mwingine. Hakuna yeyote anayelazimishwa au kushikiwa fimbo kupenda. Mapenzi huwa yanazuka tu na wala hayajulikani yametokea wapi.

Mtu anaweza kumpenda yeyote yule bila ya kuwa na kitu chochote kile ambacho kimemvutia. Yeyote anayempenda mtu kwa sababu ya kitu, basi penzi lina matatizo hilo. Siku kitu alichompendeza kitatoweka, mapenzi yanakufa kifo cha asili.

Mapenzi ni hisia tu. Mwanamume anaweza kuwaona wanawake hata 100, lakini akatokea mmoja akavutiwa naye na anayempenda atashindwa kuainisha ni nini haswa alichompendea. Anaweza kubabaisha tu lakini ukweli kitu halisi kinakuwa kwenye ubongo wake.

Mwanamke naye anaweza kutongozwa na wanaume hata 100, akawakataa wote. Akatokea mmoja tu wa 101, akamkubali kwa sababu ambazo anaweza kuziainisha, lakini ukizifutilia unaweza kukuta sifa hizo hata aliowakataa wanazo.

Amemkubali kwa sababu ambazo hata yeye mwenyewe hazifahamu vizuri. Ni hisia tu. Kwa maana hiyo mapenzi ya mtu yapo kwa mtu mwenyewe. Ziko tabia za baadhi ya watu kujifanya walimu wa mapenzi ya watu. Si wanawake si wanaume.

"Kwa nini unampenda yule? Ana nini yule ambacho atakupa wewe? Masikini yule, hana kitu yule. Kwanza ana wanawake wengi, mimi mwenyewe ameshawahi kunitongoza nikamtataa."

Ni baadhi ya maneno ambayo hutoka kwa baadhi ya wanawake ambao hao kazi yao kuingilia hisia na mapenzi za wenzao.

"Yaani ukimkubali nitakuona wewe hamna kitu kabisa shoga yangu, mkubali fulani, yule ana pesa, anakupenda na anakujali." Atampigia debe mwanaume mwingine ambaye labda humpa pesa kwa ajili ya kulaisha mambo.

Asiye na msimamo anaweza kumkataa mwanamume anayempenda kwa sababu za kuambiwa na kungukia kwa aliyelazimishwa kwa sababu ya matakwa au faida ya mtu mwingine.

Wanaume nao ni hivyo hivyo, baadhi yao wanatabia ya kwenda kwa wanawake na kuwalaumu kwa kuwapenda watu wengine.

"Yule atakwambia nini? Hana pesa, ana matatizo kibao, wewe tupende watu kama sisi."

Hawa ni baadhi ya wanaume kwenye tabia hiyo. Kama mwanamke huna msimamo unaweza ukamuacha wako anayekupenda kwa dhati ukaangukia kwake, ambaye hapendi ila anatamani tu.

Wako pia wafitini ambao wanawagombanisha hata watu walio kwenye ndoa. Ndoa nyingi zimevunjika kwa sababu ya watu wa aina hiyo na kuwaacha watoto wanateseka, hawasomi, wanahangaika na wengi wamekuwa ombaomba kisa maneno ya uongo ya kuambiwa.

Ndiyo maana wanandoa na wapenzi siku zote wanaambiwa wasisikilize maneno ya pembeni, ni mabaya sasa. Waamuzi wa penzi lenu ni wao wenyewe. Walipopendana walikuwa wawili tu, iweje leo mtu wa tatu awe mwamuzi wa penzi? Kataa.

Kupendana au kuachana iwe kwa sababu ya sababu zenu wenyewe binafsi na si ushauri au maneno ya watu. Wanamuziki wa dansi wamekuwa wakishauri kwa miaka mingi kuhusu hilo.

Leo tunaangalia wimbo uitwao 'Wajifanya Wajua' uliopigwa na bendi ndogo tu ya Tanga, Amboni Jazz. Pamoja na udogo wake ilifyatua wimbo huo ulioondokea kuwa maarufu, huku mashabiki wakibatiza jina la 'Kidomidomi.' Neno hilo limetumiwa kwenye wimbo huo likiwa na maana ya kidomodomo, likaleta ladha kubwa kwenye wimbo huo.

Katika wimbo huo, mtunzi anamjia juu dada mmoja mmoja mwenye tabia ya kidomodomo na kufitinisha mapenzi ya watu. Wakamwambia maneno haya kwenye wimbo waliouita, 'Kidomidomi.'

Ni kisa cha kweli ambapo mmoja wa wanamuziki hao walimpenda dada mmoja, lakini baada ya watu kuona mapenzi yameanza wakaanza fitina kama kawaida kiasi cha kuyateteresha.

Ilibidi jamaa amfuate mwanamke mmoja anayedaiwa kuwa ndiye kizabizabina na kumpasulia waziwazi aache tabi ya ya ufitini kwani siyo nzuri na anaweza kuadhirika siku moja.

"Wewe wajifanya wajua we dada. Unakuwa mwalimu wa wapenzi wa watu. Mimi nakukanywa, usiwe kidomidomi, utakuja adhirika ulimwenguni humu.

Usipende kashifu watu kwa wapenzi wao, utakuja adhirika dada mitaani, huko si kujenga dada ni kubomoa, mimi sikushauri kitu we dada endelea."

Ni wimbo uliokuwa na maneno mafupi, lakini yenye uzito mkubwa kwa watu wenye tabia kama hiyo.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

## Nyuma ya Pazia-7

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

AFANDE mimi naogopa kwa sababu watekaji wameniambia mambo mengi ambayo yamenitisha. Wameniambia hizi pesa ni za polisi nilizowapelekea, hawazitaki kwa sababu zina namba ambazo mnazinakili, hivyo mtawakamata hata kama wakifanikiwa kuzichukua. Wanataka ambazo ndugu tutachanga wenyewe. Na wameniambia kama nikiwaambia watamchinja mtoto wangu ni kuambia tu sehemu ambayo maiti yake wataitupa." Hata hivyo afande Chacha alimhakikishia kuwa Jeshi la Polisi litatumia nguvu, ujanja, weledi na raslimali zote walizonazo ili kumuokoa mtoto kutoka mikononi mwa watekaji.

Hilo lilimtia moyo na kuamua kumwambia kila kitu. Afande Chacha aliwatia moyo Macky pamoja na mzazi mwenzake Dora kuwa wasihuzunike, mtoto atapatikana.

"Kama yupo hai kama ulivyosema na wewe mwenyewe umemsikia kwenye simu, basi hao nia yao ni pesa tu. Safari hii hatutochukua pesa za polisi. Kwa sababu za polisi ni mpya sana. Tutachukua kwa mtu mmoja hivi, atatuazima, tena tutachukua zile zilizochakaa ili wasijue kama zetu halafu utawapelekea. Kwa mara ya kwanza hatutumia simu kuwasiliana kuhusu jambo hili, tumeitaka hapa. Tumeamua pia kutomwambia Mwalimu Mkuu kuhusu hili suala. Ni kwa sababu mara ya kwanza habari zilivuja zikafika kwa watekaji. Safari hii tumeamua kama Jeshi la Polisi siri ibaki kwa wazazi na sisi polisi ili tuone nini kitatokea. Siyo kama tunamtuhumu Mwalimu Kisanga, hapana, ila inawezekana kuna watu wa karibu anawafahamu anaongea nao, inaweza ikawa ndiyo watekaji, au wana uhusiano nao, maana utekaji umetokea kwenye shule yake." Afande Chaha aliwaambia wazazi hao jinsi walivyoamua kutovujisha siri.

"Na nyinyi msimwambie chochote kile kuhusu hili, na siyo huyo tu mwalimu, msizungumze chochote kwa ndugu zenu na majirani ili tuone jaribio la pili la kuwakamata watekaji kama litafanikiwa," alisema afande Chacha.

*****************************************

Saa sita usiku akiwa na mkoba wake wa pesa kiasi cha Sh.Milioni 15 begani. Alikuwa ameteremka kwenye basi kwenye kituo cha Magomeni Mikumi. Hakukuwa na watu wengi sana, ingawa walikuwepo baadhi wachache walevi, wanaotoka kwenye starehe na wateja wa chips.



**"Ndugu yangu nadhani wewe hatuelewani. Kila siku nakwambia usiwaambie askari siku ya kuleta pesa... "Sijawaambia" Akaropoka Macky. Alisikia sauti inayomsemesha ikicheza kwa dhihaka. "Hivi unajua unachokiongea wewe? Tulikwambia sisi tuna mtandao mpana.**

Alianza kuambaambaa upande wa kushoto wa barabara ya Kawawa kuelekea kwenye makutano ya barabara hiyo na Kigogo. Kila alipokuwa anavuta hatua mbele ndipo watu walipokuwa wanazidi kupungua na kujiona yupo peke yake.

Alifika kwenye mteremko ambao juu yake kulikuwa na daraja akashuka taratibu. Alikokuwa akielekea hakukuwa na taa nyingi. Na zilizokuwepo pembeni ya barabara zilikuwa hafifu. Ilikuwa ni hali ya kuogofya, lakini tayari alishaanza kuzoea mazingira kama hayo.

Ile hali aliyoiona siku ya kwanza pale kwenye mteremko wa Kinondoni Mkwajuni ulimomaza na kumfanya kitu woga ukae pembeni. Pia alikuwa hakuwa peke yake, bali maafande walikuwa nyuma yake wakimlinda kwa chochote ambacho kinaweza kumtokea.

Alipofika katikati ya mtereko alikuta daraja ambalo linatenganisha Magomeni na Kigogo. Ramani ilionyesha hapo ndipo kulipokusudiwa. Haikuhitajika kupanda kilima kwenda kwenye mzunguko wa makutano ya barabara ya Kawawa na Kigogo. Alikata kushoto kutoka kwenye njia ya watembeayo kwa miguu aliyokuwa akiifuata.

Wadudu walikuwa wanarukaruka kutoka kwenye majani wengine wakimpiga machoni. Kulikuwa na maeneo yenye maji, hivyo kuna wadudu ambao walikuwa kama wanawaka taa na kuzima, maarufu kama vimulimuli.

Chura nao hawakuwa nyuma, waliendelea kulia na kuhanikiza, lakini kila alipokuwa akipiga hatua kwenda mbili sauti zao zilipungua. Alipofikisha hatua tatu tu kabla ya kufika simu iliita. Akashtuka. Alijua kabisa wanaopiga ni wale wake watekaji. Ni staili kama ile ile iliyotokea Kinondoni Mkwajuni.

"Ndugu yangu nadhani wewe hatuelewani. Kila siku nakwambia usiwaambie askari siku ya kuleta pesa... "Sijawaambia" Akaropoka Macky. Alisikia sauti inayomsemesha ikicheza kwa dhihaka. "Hivi unajua unachokiongea wewe? Tulikwambia sisi tuna mtandao mpana. Kwanza kabisa tulikwambia usiwaambie polisi, ukaja nao kule Mkwajuni. Tena na pesa zilikuwa za mtego. Tukakukanya. Lakini umeenda tena kukwambia. Walicjobadilisha safari hii ni kwamba hizo pesa wamezikusanya tu kutoka kwa watu mbalimbali. Wamekusanya pesa chakavu ili kutuzuga. Na tayari wapo nyuma yako, wanakulinda. Hawapo mbali kutoka hapo ulipo. Wanachotaka ni kwamba ukishatoka tu waje kutukamata. Isingekuwa tuna mtandao mpana tungekamatwa zamani sana. Nadhani hutaki urafiki na sisi. Tumekuvumilia sana, lakini naona unatufanyia masihara. Kwa taarifa yako, kesho saa kama hizi uje hapo hapo, utakuta maiti ya mtoto wako." "Hapana hapana ha..." Alikataa Macky kwa sauti. Awali alikuwa akizungumza tararibu kutokana na mazingira yenyewe aliyokuwepo. Suala la mtoto wake kuuawa lilimshtua na kuamua kuongea kwa sauti. Wakati akitaka kuomba msamaha, tayari simu ilikuwa imekatwa kitambo.

Alijua hatompigia tena leo na si kwenye namba hiyo tena. Hata yeye akijaribu kupokea haitopatikana tena kama kawaida yao.

*********************************

Si Macky na mzazi mwenzake Dora walioonekana kustushwa na hilo, bali hata Jeshi la Polisi. Mwalimu Kisanga ametengwa kwenye mpango wa pili wa kupeleka pesa kwa watekaji, kwa nini wamefahamu?

"Tena leo wameniambia niende pale pale nilipoenda jana nikachukue maiti ya mwanangu..." Alisema Macky huku akitokwa machozi.

Afande Chacha na wenzake walimbembeleza na kumhakikishia hawawezi kufanya hivyo, ilikuwa ni harira zao tu baada ya kukosa pesa.

Dora yeye aligaragara kwenye sakafu ya ofisini, ilibidi waitwe askari watatu wa kile waje kumwinua na kumpeleka ofisi nyingine kwa ajili ya kumbembeleza na kumliwaza.

"Mama mwanangu watamuua leo." Alilia na kuomboleza baada ya kusikia maneno kutoka kwa mzazi mwenzake.

"Unasikia Macky. Sisi tuna uzoefu katika kazi hii kwa miaka mingi. Tayari lengo la hawa watu siyo kuua, siyo viungo vya binadamu. Hawa wanachohitaji ni pesa. Yaani kuwepo hai kwa mtoto kwao wana matumaini makubwa ya pesa. Kifo cha mtoto wako ina maana biashara yote ya kupata pesa kwao itakuwa imekwisha. Hawawezi asilani kwa sababu bado wana nafasi ya kupata pesa kwani mtoto yupo mikononi mwao." Maneno hayo yalimfariji Macky. Aliona kuwa ni kweli kabisa watekaji bado watakuwa wanahitaji pesa kutoka kwake, hivyo hawatumdhuru mtoto kwa sababu wakifanya hivyo, hawatoipata tena.

"Sasa kwa nini wanajua? Kwa nini wanapata habari? Kwa nini kila tunachofanya wanajua? Yaani wale jamaa inaonekana kama hata kama tukifanya kikao hapa wanajua." Akaongea Macky kwa sauti ya msisitizo iliyowashtua maaskari wengine, wakatazamana.

**Itaendelea Jumapili**



# ASANTE TESA UMETUTENDEA HAKI

• Wasanii watazidi kukulilia

TASNIA ya filamu nchini imegubikwa na huzini baada ya kumpoteza mwigizaji mkongwe, Grace Mapunda, maarufu kama Tesa, ambaye amefariki dunia usiku wa kuamkia jana.

Tesa alifariki katika Hospitali ya Mwananyamala Jijini Dar es Salaam alipokuwa anapatiwa matibabu baada ya kuugua kwa siku kadhaa.

Mdogo wa marehemu, Mchungaji Moses Mapunda, alisema dada yake alikuwa akiugua ugonjwa wa kisukari, lakini haikuwa ya muda mrefu.

Alisema alianza kupata changamoto wiki iliyopita na walimpeleka katika hospitali moja ya Buguruni kupata matibabu, lakini hali yake haikuwa sawa na ndipo walimfikisha hospitali ya Sinza na hatimaye Mwananyamala ambako alipatiwa huduma kwa siku mbili kabla ya kufariki dunia.

Aidha, Aziz Ahmed ambaye alikuwa akifanya naye kazi kama mwongozaji wa tamthilia, alisema Tesa msiba utakuwa nyumbani kwake Sinza Vatcan na taratibu zote za mazishi zitatolewa baada ya kufanyika vikao.

Grace amefanya vizuri katika Sanaa ya uigizaji akianzia katika tamthilia zilizorushwa na kituo cha televisheni cha ITV, hadi anafariki alikuwa miongoni mwa waigizaji maarufu katika tamthilia ya Huba.

Baadhi ya wasanii maarufu wamemwelezea Tesa kama msanii asiyekata tamaa, kuondoka kwake kumeacha pengo kubwa.

Jacob Steven maarufu kama JB, amesema Grace ni miongoni mwa wasanii aliofanya nao kazi kwa karibu.

"Tanzania imepoteza mmoja kati ya waigizaji bora kuwahi kutokea. Namshukuru sana Mungu kwa zawadi ya maisha yako... Nitakosa ucheshi wako, uigizaji wako mahiri lakini kubwa sauti yako," ameandika JB kupitia ukurasa wake wa Instagram.

Wema Sepetu, kupitia ukurasa wake wa Instagram aliandika kuwa kifo ni jambo la siri kubwa na alimuombea kwa Mungu ampe pumziko la Amani.

Upande wa Steve Nyerere, aliandika kwamba "Umelala Grace Mapunda, Mapenzi ya Mungu hayana makosa, mwendo umemaliza, kipaji chako kwenye tasnia kinabaki kama alama, tutaonana baadaye,"

# SQUID GAME 2 HAKUNA KULALA



MSIMU wa pili wa filamu ya Squid Game, unatarajiwa kuzinduliwa Desemba 26, mwaka huu kukiwa na maboresho kadhaa ambayo yataifanya kazi hiyo kuwa bora zaidi duniani.

Kulingana na mtayarishaji Hwang Dong-hyuk, toleo la filamu hiyo litajumuisha mastaa kadhaa na vipande vingi vitakavyoleta msisimko wa kipekee.

Hwang alisema kwamba mashabiki wa Squid Game hawatakuwa na muda wa kulala kwani msimu wa tatu tayari uko katika hatua ya utayarishaji na itatoka mwakani kwa lugha zote kubwa.

Gi-hun, ambaye alinusurika kifo katika msimu wa kwanza, atarejea kwenye mchezo, lakini huko kutakuwa na kitimtim kisicho cha kawaida.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PSG, MADRID VITANI

KLABU ya Paris St-Germain imeungana na Real Madrid katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa kulia wa Liverpool ambaye ni raia wa England, Trent Alexander-Arnold, mwenye umri wa miaka 26. (**Mail**)

### DEDIC KUMRITHI TRENT

LIVERPOOL wameulizia kuhusu beki wa kulia wa RB Salzburg na Timu ya Taifa ya Bosnia na Herzegovina, Amar Dedic, ambaye anatarajiwa kuchukua nafasi ya Trent Alexander-Arnold. (**Caught Offside**)

### WOLVES SOKONI JANUARI

WOLVES wamemfanya kiungo mkabaji wa Watford na Timu ya Taifa ya Georgia, Giorgi Chakvetadze, mwenye umri wa miaka miaka 25, kuwa mchezaji wanayemlenga zaidi ifikapo Januari. (**Sun**)

### ALONSO ATAJWA MADRID

RAIS wa Real Madrid, Florentino Perez, anaandaa misingi ya nani atakayechukua nafasi ya Kocha, Carlo Ancelotti, msimu ujao huku akimpigia debe, Xabi Alonso wa Bayer Leverkusen. (**Sport**)

### BALOTELLI ATUA GENOA

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Timu ya Taifa ya Italia, Mario Balotelli, mwenye umri wa miaka 34, jana alifanyiwa vipimo vya matibabu kabla ya kusajiliwa rasmi na klabu ya Serie A ya Genoa. (**Fabrizio Romano**)

### LOOKMAN AKARIBIA EPL

KLABU ya West Ham inavutiwa na mshambuliaji wa Atalanta na Timu ya Taifa ya Nigeria, Ademola Lookman, mwenye umri wa miaka 27, huku Kocha, Julen Lopetegui, akitumaini kuimarisha safu yake ya mashambulizi ifikapo Januari. (**GiveMeSport**)

### GVARDIOL, CITY SAFI

KLABU ya Manchester City inajiandaa kumpa mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 22, mkataba ulioboreshwa wenye thamani ya pauni 150,000 kwa wiki ili kuongeza muda wake wa kukaa Etihad hadi mwaka 2030. (**Star**)

### PALMER ANOGEWA CHELSEA

KIUNGO mshambuliaji wa England na Chelsea Cole, Palmer, mwenye umi wa miaka 22, bado anajitolea kwa The Blues licha ya kuhusishwa na kutaka kuondoka, ikiwa ni pamoja na kurejea Manchester City. (**Football Insider**)

### CHIESA KUREJEA ITALIA

AC Milan imeonyesha nia ya kumsajili winga wa Liverpool na Timu ya Taifa ya Italia, Federico Chiesa, mwenye umri wa miaka 27. (**Caught Offside**).

### HUMMELS NJIA MOJA

BEKI wa zamani wa Ujerumani, Mats Hummels, mwenye umri wa miaka 35, anaweza kuondoka AS Roma katika dirisha la Januari licha ya kujiunga na klabu hiyo ya Serie A kama mchezaji huru msimu wa joto. (**Nicolo Schira**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AFUNGUKA ANATAKA UBINGWA

**LONDON,** England

Kocha huyo asema Arsenal bado wako katika mbio za kuwania...

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema kikosi chake bado hakijaondoka katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu England licha ya matokeo mabaya ya hivi karibuni.

Arteta ambaye kikosi chake kimekuwa kikitoa upinzani mkali kwa mabingwa watetezi, Manchester City kwa misimu miwili iliyopita aliulizwa juu ya tofauti ya alama zilizopo kati yao na vinara wa ligi hiyo, Manchester City na Liverpool ambao wanaonekana kutaka kitu msimu huu.

"Kama unataka kuwa wa kwanza inabidi kushinda kila mchezo ili kuwa wa kwanza. Tunajua namna ambavyo tunapaswa kucheza kukabiliana na ushindani msimu huu, Hatujapoteana." amesema

"Tunajua mchezo wa kesho (leo) ni mgumu kiasi gani, tumejiandaa na tutakabiliana na kila lijalo kesho (leo), tuko tayari kabisa." ameongeza


**Washikabunduki hao wapo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi, wako nyuma ya vinara Manchester City baada ya kuduwazwa kwa mabao 2-0 na Bournemouth na baadaye kutoka sare ya 2-2 na Liverpool.**

Arteta amesema pia bado atawakosa beki Riccardo Calafiori na Martin Odegaard, huku Takehiro Tomiyasu akiwa bado hayupo klabuni.

Arteta pia hana uhakika kuhusu wa kupatikana kwa Ben White lakini Gabriel Magalhaes anaweza kurejea dimbani.

Newcastle United wako nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi, bila ushindi wowote katika mechi zao tano zilizopita, lakini Arteta ametahadharisha bado wanaweza kuwa tishio.

# NEYMAR ATEMWA BRAZIL




**SAO PAULO,** Brazil

MSHAMBULIAJI wa Al Hilal, Neymar na Endrick wa Real Madrid wameachwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil kitakachoshiriki mechi zijazo kwa ajili ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Venezuela na Uruguay.

Endrick mwenye umri wa miaka 18, ameichezea Madrid kwa dakika 107 pekee na hajashiriki katika michezo minne ya mwisho za timu yake.

Neymar (32), alirejea kuichezea Al Hilal Oktoba 21, mwaka huu baada ya kukosekana kwa mwaka mzima kutokana na jeraha.

"Tuliamua kutomleta ili tusiharakishe mambo," alisema Kocha wa Brazil, Dorival Junior.

"Amepona kabisa, lakini alikuwa na dakika chache tu, ambazo zilielemea sana uamuzi huo."

Neymar, ambaye ndiye mfungaji bora wa muda wote wa Brazil, aliichezea nchi yake mara ya mwisho Oktoba 17, mwaka jana mchezo ambao alipata jeraha baya la goti la kushoto.

"Alikuwa tayari kuwa hapa lakini pia alielewa hali, hali aliyonayo, ukosefu wa dakika uwanjani.

"Tunapaswa kuheshimu mchakato wa klabu. Mchezaji wa kiwango chake huwa ana furaha ya kuwa hapa. Hili ni muhimu sana kwetu, ingawa hayuko katika hali kamili."

Neymar atalazimika kusubiri hadi mechi ya kufuzu fainali ya Kombe la Dunia itakayochezwa Machi, 2025 dhidi ya Colombia na Argentina ili kurejea katika timu ya taifa.

Mshambuliaji wa Real Madrid, Vinícius Júnior, amerejea katika kikosi hicho baada ya kukosa mechi za kufuzu za Oktoba kutokana na jeraha la shingo.

Vinícius anajiunga na kikosi kufuatia wiki ya kusikitisha ambayo ilimfanya kukosa tuzo ya Ballon d'Or, Mbrazil huyo alimaliza nyuma ya Rodri wa Manchester City.

"Nilizungumza naye siku iliyopita kwa sababu ninataka kuzungumza naye kibinafsi," alisema Dorival kuhusu Vinícius.

"Kwa maoni yangu, hali isiyo ya haki, haswa kwa sababu ni tuzo ya mtu binafsi. Hakuna dhidi ya yeyote aliyeshinda tuzo, kinyume kabisa, ni kutambuliwa kwa mmoja wa wachezaji wakubwa wa mpira wa miguu wa Hispania, lakini Vinícius, kwa kazi aliyoifanya inapaswa kupokea tahadhari tofauti.

"Lakini tuzo kubwa zaidi ambayo Vinícius alishinda ilikuwa kutambuliwa na heshima ya watu wake. Idadi kubwa ya watu wa Brazil walitambua dhuluma ambayo ilifanywa kwa mchezaji ambaye angeweza kupokea tuzo hiyo kwa kustahili."

Kinda aliyetimkia Chelsea, Estêvão Willian, ambaye aliachwa nje ya timu kwa ajili ya mechi za kufuzu Oktoba, ameingia kwenye kikosi cha wachezaji 23.

Estêvão mwenye umri wa miaka 17 amefunga mabao 11 katika ligi akiwa na Palmeiras na ndiye mfungaji anayeongoza katika Ligi Kuu ya Brazil, Serie A, pamoja na Pedro Guilherme wa Flamengo.

Winga wa Manchester City, Savinho, ambaye alitolewa nje kwa machela wakati wa kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Tottenham Hotspur kwenye Kombe la Carabao Jumatano kutokana na jeraha linaloshukiwa la kifundo cha mguu wa kulia, pia amejumuishwa.

Brazil iko katika nafasi ya nne kwenye jedwali la kufuzu kwa Kombe la Dunia la Amerika Kusini, pointi nne nyuma ya vinara Argentina baada ya michezo 10.

Brazil itacheza na Venezuela Novemba 14, mwaka huu na kuwakaribisha Uruguay siku tano baadaye.

Timu sita za juu zitafuzu moja kwa moja kwa Kombe la Dunia la 2026, huku timu inayoshika nafasi ya saba ikiingia kwenye mchujo.

Kikosi cha Brazil

Makipa: Bento (Al Nassr), Éderson (Manchester City), Weverton (Palmeiras)

Mabeki: Danilo (Juventus), Vanderson (Monaco), Abner (Lyon), Guilherme Arana (Atlético-MG), Éder Militão (Real Madrid), Gabriel Magalhães (Arsenal), Marquinhos (Paris Saint-Germain), Murillo (Nottingham Forest ).

Viungo: André (Wolverhampton), Andreas Pereira (Fulham), Bruno Guimarães (Newcastle), Gerson (Flamengo), Lucas Paquetá (West Ham United) na Raphinha (Barcelona).

Washambuliaji: Estevão (Palmeiras), Igor Jesus (Botafogo), Luiz Henrique (Botafogo), Rodrygo (Real Madrid), Savinho (Manchester City) na Vinícius (Real Madrid)

## Ten Hag awashukuru mshabiki Man United

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag amewashukuru mashabiki wa Manchester United kwa uungwaji mkono wao katika maoni yake ya kwanza hadharani tangu atimuliwe kama kocha wa klabu hiyo ya Ligi Kuu England Jumatatu iliyopita.

Ten Hag alifukuzwa kazi baada ya kuifundisha Old Trafford kwa zaidi ya misimu miwili, huku United ikishika nafasi ya 14 kwenye jedwali la Ligi Kuu England baada ya kupoteza michezo minne kati ya tisa ya kwanza.

Kocha huyo Mholanzi aliiongoza United kutwaa Kombe la Carabao na Kombe la FA lakini akasikitika ndoto yake ya kuleta mataji zaidi kwa mashabiki wa United imefikia kikomo.

"Nianze kwa kuwashukuru. Asante kwa kila mara kwa ajili ya klabu," alisema katika barua ya wazi iliyotolewa kupitia wakala wake wa SEG Football.

"Ikiwa ni mechi ya mbali au mechi ngumu Old Trafford, usaidizi wenu umekuwa mkubwa. Mazingira ya Old Trafford yamekuwa ya kusisimua kila mara, asante kwanu.

Aliongeza: "Nataka kuwashukuru kwa kunipa hisia hii na kwa msaada wenu. Pia nataka kuwashukuru wafanyakazi katika kila idara ya klabu kwa msaada wao usioyumba katika nyakati nzuri na mbaya.

"Tulishinda mataji mawili mafanikio ambayo nitayathamini kwa maisha yangu yote. Bila shaka, ndoto yangu ilikuwa kuleta mataji zaidi. Kwa bahati mbaya, ndoto hiyo imefikia kikomo."

United ilithibitisha Ijumaa Kocha wa Sporting CP, Rúben Amorim, atachukua nafasi ya Ten Hag.

Kwa muda, United itaongozwa na aliyekuwa msaidizi wa Ten Hag, Ruud van Nistelrooy.

# Conte: Napoli ubingwa bado

**NAPLES,** Italia

KLABU ya Napoli ndio washika kasi wa kustaajabisha katika Serie A msimu huu, lakini ikiwa wanataka kusalia kileleni na kutwaa ubingwa basi inahitajika kazi zaidi, kwa mujibu wa Kocha, Antonio Conte.

Msimu uliopita Napoli ilimaliza katika nafasi ya 10 ambayo iligharimu kazi za makocha wawili.

Utawala wa Conte ulianza kwa kufungwa mabao 3-0 dhidi ya Hellas Verona siku ya ufunguzi wa kampeni, huku kocha mpya akiita timu yake kuwa kazi inaendelea.

Tangu wakati huo, Napoli hawajafungwa katika michezo tisa, wakishinda nane na kuruhusu mabao mawili pekee na kufungua pengo la pointi nne kileleni dhidi ya mabingwa watetezi, Inter Milan.

Alipoulizwa katika mkutano na waandishi wa habari ikiwa kushinda taji msimu huu itakuwa muujiza, Conte alisema: "Mimi ni mtu wa imani, hata kwa vitendo, na ninamjua mtu mmoja tu anayefanya.

"Siku zote huwa naomba hata kwa timu iwe vizuri, pamoja na familia yangu pia kuna dua ya kuwaombea wachezaji.

"Lazima tufanye kazi, sote, kuanzia kwa mpishi na mtu wa vifaa kuunda kitu kizuri ambacho kinaweza kutoa alama za ziada kwenye ubingwa.

"Hatuwezi kufanya makosa yoyote katika hili, hatuko katika nafasi ya kufanya makosa. Kisha, miujiza ya soka imetokea mara kwa mara, lakini unapaswa kufanya kazi ili kutumaini itatokea, haitoshi kuomba."

Leo Napoli inawakaribisha Atalanta, ambao walipoteza mechi tatu kati ya tano za mwanzo lakini sasa wamepanda hadi nafasi ya tatu kwenye jedwali baada ya kushinda mara nne mfululizo na kutwaa ubingwa wa Ligi ya Europa msimu uliopita chini ya Gian Piero Gasperini, kocha wao tangu 2016.

"Wamekuwa kwenye Ligi ya Mabingwa kwa miaka, ni timu ambayo leo lazima ihesabiwe miongoni mwa timu zenye nguvu, bila shaka," Conte aliongeza.

HABARI MICHEZO

# STARS KAMILI KUIKABILI SUDAN, KIINGILIO BURE

Na Somoe Ng'itu

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) inatarajia kuwakaribisha Sudan katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Stars inahitaji ushindi wa mabao 2-0 na kuendelea, ili kuiondoa Sudan katika mashindano hayo kufuatia kufungwa bao 1-0 katika mchezo wa kwanza uliochezwa nchini Mauritania wiki iliyopita.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Stars, Bakari Shime, alisema kikosi chake kipo imara na ana matumaini ya kupata ushindi kutokana na kiwango bora kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika mchezo wa kwanza.

"Wengi walikuwa wanacheza kwa mara ya kwanza mechi ya kimataifa, lakini walicheza vizuri mno kama ni wazoefu, tena walikuwa ugenini, hii inaonyesha wanaweza kabisa kucheza mbele ya mashabiki wao na kupata ushindi," alisema Shime.

Kocha huyo aliongeza licha ya kuwa nyumbani wanatarajia mechi hiyo pia itakuwa na ushindani kwa sababu wapinzani wao wanahitaji kusonga mbele.

Naye Nahodha wa timu hiyo, Aishi Manula, alisema wako katika mapambano licha ya Tanzania kupata tiketi ya kushiriki fainali hizo.

Manula alisema wachezaji wa timu hiyo wanataka kutumia mchezo huo kuonyesha viwango vyao.

"Tunataka kuonyesha hatima yetu nzuri ya baadaye, kuna vijana ambao wanakiu ya kufanya vizuri katika mchezo huu, tunawakaribisha Watanzania waje kufurahia ili tuwape matokeo chanya," alisema Manula.

Aliongeza watapambana kuhakikisha wanashinda kwenye uwanja wa nyumbani na sasa ni wakati wa kuondoka mawazo ya kutopata ushindi nyumbani.

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limewataka mashabiki wengi kujitokeza kwa ajili ya kuishangilia Stars na kutangaza hakutakiwa na kiingilio chochote katika mechi hiyo.

Tanzania, Kenya na Uganda ni wenyeji wa fainali hizo mwakani, ambapo Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), limezipa nafasi hiyo kama majaribio ya kuandaa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwaka 2027 (AFCON 2027).




Wachezaji wa Timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 ya Yanga wakishangilia baada ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya TFF U-17 2024. Yanga ilitwaa taji hiyo kufuatia ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya TDS U-15 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. **PICHA: TFF**

# New Amaan Complex kufungwa

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

UWANJA wa soka wa New Amaan Complex, visiwani hapa unatarajiwa kufungwa kuanzia kesho kwa muda ili kuruhusu mchakato wa ukarabati kufanyika, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF),Issa Kassim, aliliambia gazeti hili jana kufuatia uamuzi huo, mechi za Ligi Kuu zilizotarajiwa kuchezwa kwenye uwanja huo sasa zitafanyika kwenye Viwanja vya Mau.

Kassim alisema kwa upande wa Pemba, mechi za Ligi Kuu sasa zitachezwa kwenye viwanja vya Finya ili pia kuruhusu ukarabati wa Uwanja wa Gombani kufanyika.

Alisema mechi za kuanzia mzunguko wa tano wa ligi hiyo zitachezwa kwenye Uwanja wa Finya na tayari taarifa zimepelekwa kwa klabu zote.

"Uwanja wa New Amaan Complex utafungwa kuanzia Novemba 4, kuanzia sasa mechi zitachezwa kwenye viwanja viwili vya Mau A na B. Ratiba ya ligi hiyo tayari imetoka tangu Jumamosi kwa ajili ya michezo ya Jumatatu Novemba 4," alisema ofisa huyo.

Kuhusu malalamiko ya viwanja vya Mau kutokuwa na ubora, Kassim alisema kwa sasa klabu zitalazimika kucheza hapo kwa sababu ni lazima maboresho yaliyopangwa yafanyike kwenye Uwanja wa New Amaan Complex.

Alisema anaamini mechi zitakazochezwa kwenye viwanja vya Mau zitakuwa chache za kukamilisha mzunguko wa kwanza na hatua ya lala salama itakayoanza Januari itafanyika New Amaan.

## Yanga: Hatujashuka..

INATOKA UK. 24

zwa fainali ya Sh. milioni moja kutokana na kuwakilishwa na Kocha Mkuu pekee katika mkutano wa Wanahabari kinyume na natakwa ya kanuni ya 17:58 ya Ligi Kuu kuhusu taratibu za mchezo, inayotaka aambatane na nahodha ama mchezaji mwenye ushawishi kikosini.

Klabu hiyo pia imepewa onyo kwa kuchelewa kufika uwanjani huku meneja wake, Walter Harrison, amefungiwa michezo mitatu na kutozwa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la kuwataka waamuzi waliochezesha mchezo wao dhidi ya Coastal Union kufanya uamuzi kwa mujibu wa wa maoni yake, akitumia kompyuta ndogo kuwaonyesha marudio ya picha mjongeo (video) ya matukio mbalimbali ya mchezo huo kama ushahidi wa yale aliyokuwa akiyalalamikia, kitendo kilichotafsiriwa na kamati kama ni kushawishi, kuleta shari au vurugu uwanjani.

## Fadlu awalalamikia waamuzi Ligi Bara

INATOKA UK. 24

linafungwa dakika yoyote ile," Fadlu alisema.

Naye Mukwala aliliambia gazeti hili amejisika furaha kufunga bao hilo na kuwafanya mashabiki wa Simba waliojazana kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika 'kupagawa' pia kwa furaha.

"Nimejisikia furaha sana mimi binafsi, ninacheza kwa ajili ya kuipigania nembo nimejisikia vizuri kuwapa furaha mashabiki wa Simba ambao muda wote wamekuwa nyuma yetu.

Mashujaa walikuwa wagumu kwa sababu walikuwa wanacheza kwao, lakini kilitupa nguvu wachezaji, sisi ndiyo tulikuwa tunacheza kama tupo nyumbani kutokana na umati mkubwa wa mashabiki uliokuwa unatushangilia. Mashujaa waliitafuta sare na wakaona wameipata, lakini sisi siku zote ni Simba," alisema straika huyo aliyesajiliwa kutoka Asante Kotoko ya Ghana.

Kocha Mkuu wa Mashujaa, Mohamed Abdallah 'Bares', alisema wachezaji wake walipambana, lakini mpira wa miguu una maajabu yake mpaka filimbi ya mwisho ipigwe ndipo unapokuwa umeisha.

"Mechi ilikuwa nzuri wachezaji wangu walipambana sana, mwisho wa siku tukubali huu ni mchezo kama haujaisha basi ujue mpo katika mechi. Hapa mwishoni tumeshindwa kukaba wachezaji kwa haraka kwenye kona wakaitumia, wenzetu walipiga kona upesi kama unavyojua ubora wa wachezaji wa timu hizi kubwa unaweza kukuhukumu, kilichojitokeza ni uwezo wa mchezaji mmoja umeamua mechi," Bares alisema.

Simba imefikisha pointi 22 kwa michezo tisa iliyocheza na kupaa hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi huku Mashujaa ikibakia na pointi zake 13 kibindoni.

# Michezo

Jumapili Novemba 3, 2024

Nipashe



Neymar atemwa Brazil

UK. 22




Mshambuliaji wa Simba, Joshua Mutale (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Mashujaa FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma juzi. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Fadlu awalalamikia waamuzi Ligi Bara

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kupata ushindi wa jioni, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davis, amesema anashangaa kuona baadhi ya waamuzi wanaionea timu yake kwa kuinyima penalti zinazostahili na kuongeza huenda wanataka kuona wachezaji wake wakivunjwa miguu.

Fadlu alisema hayo baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake dhidi ya Mashujaa FC, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika na kuondoka na ushindi wa bao 1-0.

Kocha huyo raia wa Afrika Kusini alisema haelewi kwa nini kinatokea kwa baadhi ya waamuzi wanaochezesha michezo yao hawachuki hatua zinazostahili na hafahamu wanafanya hivyo kwa kutojua au kuna jambo lingine.

"Inawezekana Simba haistahili kupewa penalti katika Ligi Kuu kwa sababu mechi dhidi ya Yanga, Kibu alifanyiwa madhambi mara mbili ndani ya eneo la hatari mwamuzi akapeta, leo (juzi) tena, Mukwala (Steven), ameangushwa ndani ya boksi lakini hatujapewa pia, nadhani waamuzi wanataka wachezaji wangu wavunjwe miguu ndiyo waone ni kweli madhambi yamefanyika," alilalamika Fadlu.

Akizungumzia mchezo wenyewe, kocha huyo anayeifundisha Simba kwa mara ya kwanza msimu huu, alisema amefurahi kuona wachezaji wake wamecheza soka safi licha ya changamoto ya uwanja.

"Nimefurahi wachezaji wangu wamecheza soka safi kwenye uwanja ambao haukuwa rafiki. Hivi ndivyo ninavyopenda wachezaji wangu wawe, wacheze soka kwa dakika zote 90 kwa sababu bao

INAENDELEA UK 23

# Yanga: Hatujashuka kiwango

## Yapigwa faini Sh. milioni 13 kutokana na makosa katika dabi...

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ya jijini, Dar es Salaam umesema kiwango cha timu yao hakijashuka na ushindani unaoonekana katika mechi za ligi hiyo wanazocheza unatokana na wapinzani wao kuimarika zaidi msimu huu, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, amepinga kile kinachozungumzwa na baadhi ya mashabiki wa soka na wachambuzi wanaodai ubora wa wachezaji wao umeshuka.

Kamwe alisema timu yao kupata ushindi wa bao moja tofauti na ushindi wa magoli mengi kama walivyokuwa wanapata katika msimu uliopita na kuongeza hawaamini huko ni kushuka ubora.

"Tunaposema Yanga imeshuka kiwango tunakuwa tumezinyima nafasi timu nyingine ambazo zinashiriki Ligi Kuu, hatujaitengeneza kwa ajili ya kufunga watu mabao matano au 10, badala yake wapinzani nao wanaimarika.

Kwa hiyo kama wapinzani wetu katika ligi wakiimarika sio kama timu yetu ni mbovu, nadhani tungekuwa hatupati matokeo ndio mngesema tumeshuka kiwango," alisema Kamwe.

Aliongeza rekodi zinaonyesha Yanga msimu uliopita ilikuwa ikifunga mabao mengi tofauti na msimu huu, lakini pia msimu huu wameshinda michezo nane mfululizo kitu ambacho hakikufanyika msimu uliopita na wavu wa timu yao bado haujaguswa.

"Tumeshinda mechi nane mfululizo, hatujaruhusu bao mpaka sasa, hii ni rekodi ambayo msimu uliopita haikuwepo, utasemaje tumeshuka kiwango?

"Ninavyoona mimi wapinzani hivi sasa wanaimarisha timu zao hasa upande wa ulinzi, makocha wao wamekuwa wakifanya kazi kubwa kuizuia Yanga, lakini watu hawafanyi hivyo wanakuja kusema tu tumeshuka kiwango," Kamwe alisema.

Msimu uliopita Yanga ilipoteza mechi ya raundi ya nne, ikifungwa mabao 2-1 dhidi ya Ihefu na ndiyo ilikuwa mara ya kwanza kuruhusu wavu wake kuguswa, baada ya kuichapa KMC mabao 5-0, ikaifunga JKT Tanzania idadi kama hiyo halafu ikapata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo, kabla ya kukutana na kipigo hicho.

Wakati huo huo, Kamati ya Uendeshaji wa Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania imeitoza Yanga faini jumla ya Sh. milioni 12 kutokana na makosa matatu waliyafanya katika mechi ya dhidi ya Simba iliyochezwa Oktoba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiibuka na ushindi bao 1-0.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Yanga imetozwa Sh. milioni 10 kwa kutumia mlango usio rasmi wa kuingilia uwanjani siku ya mchezo kinyume na kanuni ya 17:62 ya Ligi Kuu.

Pia Yanga imetozwa faini ya Sh. milioni moja kwa kosa la kukataa kutumia chumba maalumu cha kubadilishia nguo kinyume na kanuni ya 17:62, na kosa la tatu imeto-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002